

MLANGO KATIKA MLANGO



Asante sana, ndugu, Ndugu Tony, na kwa marafiki wote, wasafiri wanaosafiri, wageni! Mnajua, hatudai kuwa ninii... Samahani.

² [Ndugu mmoja mimbarani anatoa taarifa kuhusu Mungu kujibu maombi ya Ndugu Branham miaka mitatu iliyopita huko Tulsa, Oklahoma, na watu wengi waliokoka katika huduma yake Brazil mwaka huo—Mh.]

³ Mungu akubariki, ndugu. Ni—ninapenda kusikia taarifa hizo za wakati watu wanaokoka, mwajua. Hilo ndilo—ndilo jambo muhimu. Nasi tuna furaha kuwa hapa na kuona wengi sana wa marafiki zetu kutoka sehemu mbalimbali za nchi. Na ndugu huyu hapa anakuja mjini sasa, nasikia, asubuhi ya leo, kwamba kifaa chake kimeshushwa hapa tayari kwa—kwa ajili ya uamsho mkubwa. Bila shaka ninaomba, ndugu, ya kwamba Yeye atawapa uamsho mkuu na watu wengi hapa mjini.

⁴ Nami nina furaha asubuhi ya leo kuwaona wengi wa marafiki zangu wahudumu. Ndugu Outlaw pale, ndio kwanza nimwone wakati niliposimama, kutoka Phoenix. Nami nina furaha sana kukuona huku chini, Ndugu—Ndugu Outlaw, ninyi ndugu kutoka Yeriko mkipanda kuja huku Yerusalemu, kututembelea. Daima tuna furaha kuwa nao. Hiyo ni kweli, Tony.

⁵ Na kwa hiyo—na kwa hiyo nikaitoa hiyo, hadi kwa Ndugu Williams, sio muda mrefu uliopita, huko Phoenix. “Mwajua,” nikasema, “Tucson, ninaishi hapa sasa, mwajua. Kwa hiyo kwa namna fulani inanibidi kupatetea mahali hapa, mnaona, juu mlimani hapa, na kuangalia chini Yeriko na kuwaona ndugu zetu. Mbona, daima sisi...”

⁶ Naye Ndugu Carl alikuwa akizungumza kuhusu wengi sana wakija maili mia moja, kutoka Phoenix huku chini. Ni wangapi waliopo hapa kutoka Jeffersonville, Indiana? Simameni. Kote kote, huku. Hiyo ni kama maili elfu mbili mia moja. Loo, Carl!

⁷ Nina furaha sana kuwa hapa na kufurahia mwangaza huu wa ajabu wa ndani ya Mwana. Mnaona, sisi huzungumza juu ya huu kuwa ni mji wa jua. Hilo ni nje. Lakini, loo, Mwana huyu wa ndani, jamani, hilo ndilo ninalofurahia.

⁸ Nimekuwa nikifurahia baraka hizi juma hili, na kuhudhuria uamsho wa Ndugu Bethany hapa, huko kwenye First Assemblies of God. Nami hakika ninamthamani askari huyu shujaa wa msalaba, mahubiri yake mazuri. Yamekuwa mengi sana kwangu, juma hili. Nikasema, “Mimi na Ndugu Bethany tuna mambo mengi sana shirika, hasa sana jinsi tunavyozipiga wei nywele

zetu, Ndugu Bethany.” Ni hivyo, basi, tunaweza kutambuana daima, popote tulipo.

⁹ Kwa hiyo tunashukuru kwa ajili ya nafasi hii kuwa hapa pamoja na Ndugu Tony. Siwezi kulitamka jina hilo, na kwa hiyo ninamwita tu “Ndugu Tony.” Samahani. Walimwita Petro, “Petro,” na Paulo, “Paulo,” na kwa hiyo huyu ni Tony. Daima mimi huwaambia, “Niiteni tu, ‘Ndugu Bill.’” Hilo ndilo mimi. . . Napenda jina hilo, “Ndugu Bill,” ama “Ndugu,” haidhuru, kuhusishwa pamoja—pamoja nanyi, kuwa ndugu.

¹⁰ Nilifurahia hicho kiamshakinywa! Kitu pekee, hakukuwako na sukari ya rojorojo ya kutosha. Ni—ni—niliishiwa. Ndipo nikaomba kutoka kwa mwanangu, nikammaliza naye, tena nikaomba kutoka kwa ndugu yao. Alikuwa na sahani ya ziada, na bado sikupata sukari ya rojorojo ya kutosha. Mwajua, mimi ni Mbaptisti. Siamini katika kunyunyizia. Ninapenda kuyabatiza kwelikweli. Ninapenda sukari ya rojorojo nyingi, nyingi sana. Nilichukua bakuli ya sukari, na hakuna nyingi sana iliyosalia ndani yake. Ilinibidi niyatie sukari kidogo, mwajua.

¹¹ Nakumbuka huko kusini, huko chini, ninaamini ilikuwa ni Alabama, nilikuwa pamoja na wa—watu wa Baptisti ya Kimishenari. Nilikuwa huko chini, nikiwa na mikutano ya uamsho. Na nilikuwa katika maskini baraza ndogo iliyowekwa wavu, upande wa nje. Basi kulikuwako na maskini dada mweusi. Akasema. . . Mwajua, nilikuwa nimehubiri kwa nguvu usiku huo, na basi ilikuwa vigumu kwangu kuamka kesho yake asubuhi. Ndipo akaniita, nami nakumbuka kuwa macho muda mrefu kutosha kumsikia akisema, “Hei, mchungaji.” Akasema, “Kipenzi, hima. Tayari nimepika magole yako mara nne, tayari, asubuhi ya leo.” Mara nne aliyapika hayo magole! Na—nayapenda. Hadithi ndogo tu, najua. Tupo hapa tu katika ushirika, mwajua.

¹² Maskini Ndugu Bosworth, ni wangapi waliopata kumjua Dk. Bosworth? Alikuwa mzee rafiki yangu sana. Aliniambia, wakati mmoja, akasema, “Ndugu Branham, unajua ushirika ni nini?”

Nami nikasema, “Na—nafikiri ninajua, daktari.”

¹³ Akasema, “Ni jamaa wawili katika meli moja.” Mwajua, hiyo ni hapa tu, ambapo wananinii. . . Na kwa hivyo hiyo ndiyo njia. Huo ni ushirika wa karibu; wa karibu, sio uliofungwa; ushirika wa karibu mmoja kwa mwingine.

¹⁴ Kumbukeni, siku moja, tukitafakari juu ya magole. Tunayaita “magole,” huko Kusini, Ndugu Bethany. Kwa hiyo sisi. . . Nilikuwa kwenye ziara ndogo ya kuvua samaki, huko New Hampshire ya kaskazini. Ndiko wanakopatikana trauti wakali na wenye mikia miraba. Nami nilikuwa na hema dogo mgongoni mwangu. Nilikuwa nimepakia huko nyuma, yapata safari ya siku moja na nusu, ambako jamaa wote miguu laini wasingeweza kwenda. Kwa hiyo nilikuwa huko nyuma

nikiwavua trauti. Loo, ni wakati wa jinsi gani niliokuwa nao! Na maskini kijihema. Basi siku moja kabla, shimo dogo la maji, loo, kulikuwako na trauti mzuri mkubwa amelala mle ndani, nami nilikuwa tu nikiwashika upesi iwezekanavyo. Nami ningemshika mmoja. . . Kama nilimwua, basi ni—ningemchukua na kumla. Lakini, kwa kawaida, ningemwachilia, kama haikumuumiza sana.

¹⁵ Na daima ningemshika nzi wangu juu ya kichaka cha kongoni nyuma yangu. Nami nikawaza, “Kesho yake asubuhi, mapema, nitachukua shoka langu na kushuka kwenda kule chini na kufyeka kichaka hicho cha kongoni,” maana ningemshika Kochamani wangu kwenye hicho—kwenye hicho kichaka cha kongoni. Kwa hiyo nikaamka mapema, nami nikawaza, “Vema, huenda nikamshika trauti mmoja ama wawili kwa ajili ya kiamshakinywa.” Nami nilikuwa peke yangu. Basi nikachukua maskini shoka langu la kale nikaenda huko chini na kufyeja kichaka hiki kidogo cha kongoni na kujivulia samaki kadhaa, nikawa njiani nikirudi.

¹⁶ Ndipo nikasikia sauti. Ilikuwa ni maskini dubu jike. Mahali hapo palijaa wao. Alikuwa ni dubu mweusi. Alikuwa na vitoto viwili. Naye alikuwa ameingia hemani mwangu. Walikuwa wameirarua kabisa. Hakuna kitu kilichosalia. Ilininii tu. . . Si yale wanayokula; ni yale wanayoangamiza. Wakisikia tu chochote kikichacharika, wa—wanakirukia, mwajua. Nalo maskini bomba la stovu yangu lilikuwa limepondwapondwa, na, vema, hakuna la kufanya ila kurudi nyuma.

¹⁷ Ndipo maskini huyo dubu jike aliponiona nikija, alitoroka na kuwaita watoto wake, ndipo mmoja wao akaja. Huyo mwingine hakuja. Vema, nilishangaa ni kwa nini hakuondoka. Vema, ni—nilikuwa na bastola ya kale iliyoingia kutu imewekwa hemani, lakini huyo dubu alikuwa ameikalia hiyo bastola. Kwa hiyo nisingetaka kumpiga risasi maskini huyo dubu, kwa vyovyote vile, na kuwaacha mayatima wawili mwituni. Kwa hiyo mimi. . . Nami hakika. . . Ukimchukua maskini mama dubu aliye na watoto, hakika atakukwaruza, wajua. Kwa—kwa namna fulani yeye hufadhaika kidogo unapoanza kuwazia utawasumbua hao watoto.

¹⁸ Kwa hiyo maskini jamaa huyu alikuwa ameketi, na ni mtoto mdogo tu wa dubu. Alionekana labda ana uzito wa pauni ishirini; pauni kumi na tano, ishirini. Ilikuwa ni mapema, walikuwa ndio kwanza watoke kubumbuwa muda kidogo. Basi jamaa huyo mdogo alikuwa ameugeza mgongo wake kwangu, ameinama kabisa, namna *hiyo*. “Vema,” nikawazia, “maskini jamaa yule anavutiwa na nini?” Basi maskini mama dubu na mtoto huyo mwingine walikuwa huko nje, naye akaendelea kumwita, wala asingemsikiliza hata kidogo.

¹⁹ Nikawaza, “Maskini jamaa yule ana shida gani?” Nikajitafutia mti wa karibu, ambao ningeupanda kama angalinifukuza. Kwa hiyo nikawaza, “Sina budi kuona ni kitu gani kimemvutia sana jamaa yule mdogo.” Kwa kawaida watatoroka. Kwa hiyo nikaendelea kwenda huku na huku, nikimwangalia, mpaka nikafika upande mmoja. Nawe ungeshangaa ni nini kilikuwa kikiendelea.

²⁰ Jamaa huyo mdogo alikuwa ameipata ndoo yangu ya sukari ya rojorojo, na—na ndoo mdogo ya nusu galoni iliyojaa sukari ya rojorojo. Naye alikuwa ameondoa kifuniko chake. Nao wanapenda utamu, kwa vyovyote vile, mwajua. Hakujua jinsi ya kuinywa. Kwa hiyo akachukua maskini wayo wake mdogo na kuuchovya na kuulamba, namna *hiyo*, mwajua, wakati alipoutoa. Naye a—asingeweza... Nikampigia makelele. Nikasema, “Toka hapo.” Ndipo akageuka. Asingeweza kuyafungua macho yake, sukari ya rojorojo ndani ya macho yake, mwajua, akiangalia, mwajua. Naye alikuwa ameifyonza ndoo hiyo akaisafisha vizuri alivyoweza.

²¹ Nami nikasimama tu na kucheka. Na wakati wowote, wakati huo sina kamera, mwajua, kupiga picha hiyo. Naye huyo hapo. Ndipo basi baada ya kumaliza kuulamba ninii, mwajua, ndoo yote, vizuri sana, akawaendea maskini yule mama na ndugu mdogo, nao wakamlamba.

²² Kwa hiyo—kwa hiyo nikawaza, “Huo ni kama mkutano mzuri wa kale wa kipentekoste, tunapoingiza mikono yetu kwenye gudulia la asali, kufikia kwenye viwiko. Kisha tunatoka, tunamwambia mtu mwingine, tunaacha walambe kidogo kutoka kwetu, mwajua. Mkutano tu wa kulamba vizuri, mwajua. Huo ndio niliofikiria maskini dubu huyo mdogo alikuwa nao.

²³ Sasa, hakuna hukumu kwake, mradi tu alikuwa akilamba sukari ya rojorojo, mwajua. Kwa hiyo hivyo ndivyo tunavyojisikia katika mkutano mzuri wa mtindo wa kale. Hakuna urasimu. Hakuna chochote, bali kwa urahisi ni kuketi tu na kulamba. Hayo ndiyo yote.

²⁴ Katika Biblia, mnajua, mchungaji alibeba mkoba mdogo ubavuni mwake. Na mara nyingi, mle ndani, angebeba asali kidogo. Basi alipompata kondoo aliyekuwa ni mgonjwa, mchungaji huyo angeenda kule, na kuminya kidogo, asali hii, juu ya jiwe la chokaa. Nao kondoo wanapenda kitu kitamu, pia, mwajua. Kwa hiyo angeenda pale, kondoo angeenda, na kuanza kulilamba jiwe hilo. Alikuwa akiilamba asali, bali wakati akiilamba asali alipata hilo jiwe la chokaa, nalo jiwe la chokaa likamsaidia kupona.

²⁵ Ninao mfuko mzima hapa uliojaa asali, nami nitaiweka juu ya ule Mwamba, Yesu Kristo, nanyi kondoo muanze tu kuulamba sasa. Nina hakika uta—utaponya magonjwa yetu yote ikiwa tu tutaulamba huo Mwamba wa kale, na Yeye

hakika atayashughulikia hayo mengine. Yeye ndiye Mponyaji wetu wa maudhi ya kimwili na ya kiroho. Yeye ni Nyinyoro ya bondeni. Na katika nyinyoro tunapata afyuni, nayo afyuni hutatua mambo yote. Inakutia tu bumbuwazi, na hivyo ndivyo Roho Mtakatifu anavyokuja. Hukuweka katika hali ya kutojali ambapo hujali ni nani anayeketi karibu ama chochote kukihusu. Huna budi kutoa mvuke basi. Jambo ndilo hilo.

²⁶ Nakumbuka maskini msichana mmoja wakati mmoja alijazwa na Roho Mtakatifu. Alikuwa ni Mmethodisi mdogo, pia. Naye alikuwa akitoa ushuhuda. Nami kamwe sitasahau lile tamshi la kifidhuli, si baya kuliko lile ninalotoa mimi. Basi alisema, “Vema, ninataka kumsifu Bwana kwa ajili ya huyu Roho Mtakatifu.” Akasema, “Kama ingalikuwa bora zaidi, ningepasuka.”

²⁷ Ninaipenda mikutano na mikusanyiko hii ya Wafanyabiashara wa Full Gospel. Nanyi mwajua, niliwekwa wakfu kwa huduma miaka michache iliyopita, kama miaka thelathini na mitano iliyopita, katika kanisa la Baptisti ya Kimishenari. Na huko nilijaribu kuwa mhudumu mwaminifu kwa Injili, na yote niliyojua kwamba yalikuwa sahihi, kwa miaka kadhaa. Ndipo basi baada ya lile ono kuu kuja . . .

²⁸ Na kamwe sikuwa nimesikia kitu kama Pentekoste. Niliwasikia wakisema kulikuwako na kundi la watakatifu wanaojibingirisha sehemu ya chini ya mji, wanaotoa udende sakafuni, kila kitu. Vema, kamwe sikuyatilia maanani hayo hata kidogo. Lakini wakati Mungu aliponiita, nilikuja miongoni mwao, nami nimeninii tu... Ilionekana kana kwamba yale yaliyokuwa moyoni mwangu, kutamani sana kitu fulani, ni kama tu kutia glavu katika mkono wenye baridi. Ni jambo tu linalofaa, nami nimelifurahia kabisa.

²⁹ Nilipokuja miongoni mwa ndugu hawa, niliona kwamba miongoni mwao ilikuwa ni kama sisi Wabaptisti. Walikuwa wamegawanyika katika madhehebu mengi mbalimbali! Jamani, wote walikuwa wa namna mbalimbali. Na baadhi yao walikuwa wakiendesha ngamia wa nundu moja, na wengine wa nundu mbili, na wengine wa nundu tatu, na wengine hakuna nundu hata kidogo. Lakini, mwajua, nikawaza, “Sitajiunga na kundi lolote lile, kwa sababu ningetambulishwa tu na kundi hilo moja. Kwa hiyo nitasimama tu kati yao na kusema, ‘Sisi ni ndugu.’”

³⁰ Ninaamini ilikuwa ni Yakobo aliyechimba kisima, nao Wafilisti wakamfukuza kutoka kwake. Ninavyokumbuka vizuri, yeye alikiita “Kijicho,” ama kitu fulani. Kisha akachimba kingine, na akasema Wafilisti walimfukuza kutoka kwake, kwa hiyo akakiita “Ugomvi.” Akachimba kingine. Akasema, “Ipo nafasi kwa ajili yetu sote.” Na hilo ndilo ninaloamini. Ipo nafasi kwa ajili yetu sote.

³¹ Na sasa mimi, kitu pekee ambacho nimejiunga nacho tangu nimekuwa katika mwenendo wa full Gospel, mimi ni mmoja wenu. Nami nafikiri ndicho kitu kilichokaribia Mbingu kuliko vyote kilichopo. Kama kuna kitu chochote kilicho karibu zaidi, nitajaribu kukipata. Bali *Hili* ndilo nimepata, nami nalipenda *Hili*. Nitadumu na *Hili* mpaka kitu fulani kilicho bora zaidi kije. Nami ninatazamia kitu kilicho bora zaidi kije. Kama vile Petro alivyosema, kwenye Siku ya Pentekoste, yeye alisema, “*Hili ni Lile.*” Na kama *hili* si *Lile*, basi nitaliweka *hili* mpaka *Lile* litakapokuja. Kwa hiyo, basi nitashikilia tu hili, maana hili ni zuri sana.

³² Halafu nikakuta kwamba hawa Wafanyabiashara Wakristo, Wafanyabiashara wa Full Gospel, walikuwa kwa njia fulani wamesimama vivyo hivyo, katika pengo, kati ya madhehebu makubwa, mazuri ya makanisa, wakijaribu ku—kuunganisha kitu fulani, ambacho kilikuwa, ni kufanya ushirika, kushindania, sio kujaribu kuvunja yoyote ya madhehebu yao, wala kuyafanya yote kuungana yawe ni moja, bali ni kuleta tu ushirika. Na hiyo ndiyo sababu nilijiunga. Basi ndilo shirika la pekee ambalo mimi ni mfuasi wake ni hili, hili la Wafanyabiashara wa Full Gospel, kwa sababu li—linajaribu kufanya kile ninachowazia ni ninii... kingekuwa huduma kuu kwa Mungu na Kanisa Lake, kuleta hisi miongoni mwetu, kwamba hatujatenganishwa. Sisi ni ndugu, na sote tulimpokea Roho Mtakatifu yule yule. Sasa, Mungu hukupa Roho Mtakatifu; anampa mtu huyo mwingine Roho Mtakatifu.

³³ Kama vile kundi la Wabranham, nina ndugu tisa, na kuna walio wanene na wafupi, warefu na wembamba, nami ni Bw. Katikati. Kwa hiyo wao—wao wanatofautiana, wengine wana nywele nyeupe, na wengine nywele nyeusi, na wengine hawana kabisa. Na kwa hiyo ningali ni Bw. Katikati. Kwa hiyo, lakini, mle ndani, sisi—sisi ni ndugu. Tulizoea kutoka nje kwenye—kwenye ua wa nyuma na kupigana. Lakini tulipofika kwenye ua wa mbele na mtu fulani amrukie yeyote wa Branham, u-hu, ilikuwa tu ni vibaya sana.

³⁴ Na kwa hiyo hivyo ndivyo nafikiri inatupasa sisi sote kujisikia, mwaona. Wakati mwingine Mungu hufanya mambo ambayo sisi... huenda tu yasionekane mazuri tu machoni petu. Lakini, hata hivyo, kama ni Mungu anayefanya, hebu na tuseme tu “amina” kwake. Mungu huyafanya, kwa vyovyote vile, mnaona. Nasi tuna—tunautazamia wakati ambapo...

³⁵ Nilikuwa nimeketi kwenye ibada ya Ndugu Bethany Jumapili iliyopita usiku, akihubri juu ya alama ya mnyama, ndipo mtu huyo akagusa jambo muhimu sana pale ambalo liliichangamsha sana nafsi yangu. Alisema ya kwamba huko chini safarini kuna jambo fulani lililo kuu zaidi linalongojea, kitu kama hicho pale, kitu ambacho Mungu anajiandaa kufanya. Ninaamini hilo, pia, kumalizia kabisa kitu hiki na kulipeleka

Kanisa Utukufuni. Ni ajabu jinsi gani! Sasa hebu na tusiwe wazembe sana sasa, hata tutaninii. . .

³⁶ Kumbukeni, Mungu kamwe habadilishi njia Zake. Yeye ni. . . hudumu, kwa sababu Neno Lake. . . Yeye ni Neno, nalo Neno Lake haliwezi kushindwa. Yeye hana kikomo. Kwa hiyo kama Mungu akifanya uamuzi juu ya jambo fulani, hauna budi kubaki hivyo daima. Hawezi kurudi nyuma na kusema, “Nilikosea.” Mnaona? Ninaweza kukosea; unaweza kukosea. Lakini, Mungu hawezi, kwa sababu Yeye hana kikomo. Mnaona? Uamuzi Wake wa kwanza ni wa Milele.

³⁷ Wakati Mungu alipompa mwanadamu kinga iliyo bora kuliko zote aliyoweza kuwa nayo kwa ajili ya ninii Yake. . . kumfungia ndani, kumzingira ndani, Mungu alimpa mwanadamu Neno Lake katika Bustani ya Edeni, Neno Lake. Naye Hawa akafanya ile pupa, ya mwisho, kuu. . . moja ya mambo ya kijinga sana aliyowahi kufanya, ama angaliweza kufanya, ilikuwa ni kuhojiana na Neno la Mungu. Hatutoi hoja; tunaliadini tu. Sasa, Mungu kamwe hajaweka kitu kingine chochote ila kuliadini Neno Lake. Hiyo ni kweli. Neno Lake, hatuna budi kukaa nyuma Yake.

³⁸ Sasa dokezo dogo tu hapa. Mnajua siku moja Biblia ilikuwa imetabiri juu ya nabii mkuu ajaye ambaye alikuwa atawakusanya Israeli pamoja. Ndipo wakati Yeye alipokuja, mnajua Yeye alipitia moja kwa moja kwa watu nao hawakujua? Ndipo basi siku moja Yesu alikuwa akizungumza na wanafunzi Wake, kasema, “Mwana wa Adamu anapanda kwenda Yerusalemu,” na kadhalika.

³⁹ Wao wakasema, “Ni kwa nini waandishi. . .” Kwa maneno mengine, waandishi wa Maandiko. “Kwa nini waandishi walisema ya kwamba Eliya hana budi kuja kwanza na kurejesha mambo yote?”

⁴⁰ Akasema, “Ninawaambia, kwa kweli Eliya atakuja kwanza. Bali nawaambia ya kwamba Eliya amekwisha kuja wala hamkujua. Mnaona, alipita moja kwa moja; hawakujua. Vivyo hivyo Mwana wa Adamu.” Walifahamu alinena juu ya Yohana Mbatizaji. Sasa, mnaona, yeye alikuwa ni kichaa tu huko chini mtoni mahali fulani, mtu wa mwituni, akijaribu kuwazamisha watu majini, kadhalika, ujumbe wa kigeni sana. Lakini huyo alikuwa ndiye mtangulizi wa Mungu. “Nayo yakapita, nao hata hawakujua.” Yesu alikuja. . . Nadhani theluthi moja ya Wayahudi kamwe hawakusikia juu ya Yohana.

⁴¹ Nadhani wakati Yesu, duniani, sio wengi mno wa Wayahudi, na moja katika mia moja ya watu wa duniani, ndio walipata kujua Yeye alikuwa hapa. Alikuwa amekuja na kuondoka.

⁴² Kanisa, ninyi Wakatoliki, jinsi mnavyojaribu vizuri kum dai Mtakatifu Patrick. Mtu yeyote aliyemjua Mtakatifu Patrick, yeye alikuwa karibu ni Mkatoliki, Katoliki ya Kirumi, kadiri nilivyo

mimi. Kwa hiyo, lakini tazameni, mtazameni Joan wa Arc, maskini yule msichana mtakatifu aliyeona maono na kadhalika. Ninyi mlifanya nini? Mlimchoma kwenye nguzo, kama mchawi. Aliondoka kabla hamjajua alikuwa ni mtakatifu. Mnaona? Mnajua nini, hilo si linge kuwa ni jambo baya sana?

⁴³ Na Yesu akasema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu, ambako watu wanane waliokolewa kwa maji.”

⁴⁴ Vipi kama leo Unyakuo ungekuja? Naye akawachukua wawili kutoka Tucson, na mmoja kutoka Phoenix, na kote ulimwenguni, kama vile Unyakuo wa dunia nzima utakavyokuwa. Na wale watakaofufuka kutoka kwa wafu wataenda kukutana na Yeye hewani, na kuchukuliwa kisiri, jambo la kisiri. Na ndipo moja ya siku hizi hukumu itashuka juu ya nchi. Mtasema, “Vema, hivi hakukupaswa kuwa na Unyakuo kwanza?”

“Umekuja tayari, nanyi hamkuutambua.”

⁴⁵ Wazieni ni watu wangapi watakaokosekana ulimwenguni leo hii, na hapatakuwapo na hata neno. Hamtajua lolote kulihusu. Kutakuwa na watu mia tano ulimwenguni leo hii watakaokosekana, nanyi hamtajua chochote juu yake.

⁴⁶ Tunaishi katika wakati wa kutisha sana. Hebu na tuzitengeneze taa zetu. Sisemi itakuwa hivyo. Ninasema, vipi kama ilikuwa? Ndipo hukumu inapiga na Unyakuo umekwisha pita. Mnaona?

“Amekuja tayari, nanyi hamkujua.”

⁴⁷ Kwa hiyo tunapokusanyika katika mikutano hii, hebu tukusanyike, sisi, kwa kusudi moja, hilo ni kumtumikia Mungu. Hebu tuyaweke maisha yetu kazini. Inatufaidi nini kuiga jambo fulani? Kwa nini tukubali kabadala wakati anga nzima zimejaa nguvu halisi za kipentekoste, na baraka? Kwa nini tukubali kabadala? Hamwezi kuzimaliza baraka za Mungu. Ombeni kwa wingi.

⁴⁸ Ungeweza kuwazia samaki mdogo, yapata urefu wa kama nusu inchi, huko nje katikati ya bahari, akisema, “Afadhali ninywe maji haya kwa unyimifu. Huenda nikaishiwa”? Sasa, hilo linasikika la kipumbavu. Vema, ni la kipumbavu kuliko hivyo, kudhania unaweza kuomaliza wema wa Mungu.

⁴⁹ Mimi, nikiangalia muda mfupi uliopita, na ni heshima kumwona yule mzee, baba na mama ya Carl Williams; mara ya kwanza nilipokuwa na majaliwa ya kuwaona, ni juavyo mimi, wakisimama. Basi wazieni, karibu umri wa miaka themanini, kitu kama hicho, na jinsi Mungu amewaweka hao mume na mke wazee. Wangeweza kuonekana kama ndugu ya Carl, sio baba yake. Naye Tony alisema mama yake alitoka kwenye gari huko nje, akaubamiza mlango, akatembea kama maskini

askari akapita. Jamani, jamani! Mnaona? Jinsi Mungu amekuwa mwema kwetu!

⁵⁰ Sasa, kama wewe si ninii—kama wewe si mfuasi wa hawa Wafanyabiashara wa Full Gospel, ninyi wanaume... Kama Mbaptisti, ninazungumza na nyinyi Wabaptisti. Kama Mmethodisti, mimi ni Mmethodisti.

⁵¹ Basi wakati mmoja nilikuwa nikihubiri huko chini Arkansas nami ningeninii... Alikuwa ni mzee mwenye mikongojo, naye alikuwa ameponywa. Aliuza penseli huko mtaani. Naye alikuwa amesimama wima usiku huo, naye alikuwa tu anachukua mkutano huo wote. Ilikuwa ni kama, loo, nadhani watu elfu tano ama sita waliokusanyika pale kwenye Jumba la Mikutano la Ukumbusho wa Robinson, naye... huko Little Rock. Naye akasema, “Mungu asifiwe kwa kuniponya.” Ilikuwa vigumu kwako kuhubiri. Ndipo mara moja akasimama. Akasema, “Hei, Ndugu Branham, ninataka kukwambia jambo fulani.”

⁵² Sasa, alikuwa tu na yubile ya ulaji bora wa kibinafsi yote peke yake. Kwa hiyo a—alikuwa tu na wakati mzuri. Alikuwa ameponywa na hilo lilimaanisha kila kitu kwake. Na kwa hiyo akasema, “Unajua...” Ilitokea kwamba, yeye alikuwa ni Mnazarayo. Ndipo akasema, “Unajua, nilikusikia ukizungumza, nami nilikuwa na hakika ulikuwa Mnazarayo.” Akasema, ndipo akasema, “Mimi pia...” Akasema, “Ndipo nikamsikia mtu fulani akisema ulikuwa Mbaptisti.” Akasema, “Nao karibu watu wako wote hapa ni Wapentekoste. Sielewi hilo mimi.”

⁵³ Nikasema, “Loo, hilo ni rahisi sana.” Nikasema, “Mimi ni Mpentekoste Mnazarayo Mbaptisti.” Jambo ndilo hilo. Hiyo ni kweli.

⁵⁴ Sisi ni Wakristo, waliozaliwa kwa Roho Wake, wakaoshwa kwa Damu Yake, wakikutazamia Kuja kwa Bwana wetu. Bwana awabariki.

⁵⁵ Kama wewe ni mfanyabiashara ama chochote zaidi, hebu nikwambie jambo fulani. Ingia ndani. Njoo, shiriki. Usishiriki tu na kundi la watu unaoweza kuwapa mikono, bali pata walicho nacho, Roho Mtakatifu. Huyu huleta ushirika halisi.

⁵⁶ Mwajua, huwezi kutengeneza chochote. Huombwi kutengeneza chochote. Kanisa haliombwi kutoa ama kutengeneza tunda. Unapaswa kulizaa tunda. Unaona? Usingeweza kumwambia—kumwambia kondoo, “Tengeneza sufu.” Acha tu awe kondoo, naye atazaa sufu. Hiyo ndiyo shida yake, tunajaribu kutengeneza kitu fulani. Usikitengeneze. Kuwa, pafanye tu ndani pawe sawa.

⁵⁷ Ungeweza kuwazia ndege mweusi ameketi pale juu na kujibandika manyoya ya tausi kwenye mabawa yake, na kusema, “Mnaona kwamba mimi ni tausi”? Yeye anajaribu kuweka kitu ndani ambacho kamwe hakikuwa ni cha kutoka ndani kwenda nje. Nasi tunapata mengi mno ya hayo miongoni mwa

makundi yetu ya Kipentekoste. Hebu na tuwe wapentekoste halisi, wa kweli, waliozaliwa mara ya pili. Nitasema sasa, ndicho kitu cha pekee nilichowahi kupata, upande huu wa Mbinguni, kilichonipa hakikisho ya kwamba dhambi zangu zimekwisha, nami nimezaliwa kwa Roho wa Mungu. Ndipo una kitu fulani, nanga ndani yako, inayoshikilia.

⁵⁸ Vema, sikukusudia kuchukua muda wenu mwingi sana. Ninajua hamna budi kwenda. Na mimi kidogo ni mmoja wa hawa hapa jamaa wa maneno mengi. Hunichukua kama saa moja kuanza, kisha ninahubiri kwa yapata saa mbili, halafu inanichukua kama saa tatu kumaliza. Na kwa hiyo si—sitachukua msimamo mkali hivyo, asubuhi ya leo, hata hivyo. Kwa hiyo tunakuthamini kuja kwenu.

⁵⁹ Na ninaishi hapa Tucson sasa, hapa katika Yerusalemu nzuri ya kale. Nami nitashuka mara moja ama mbili, Ndugu Tony, Bwana akipenda, kusaidia huku, na kuhudhuria miamsho yenu nyote ya wote. Kwenu ninyi ndugu wahudumu, kamwe sikuja hapa kujenga kanisa lolote. Nimekuja hapa kusaidia lile ambalo tayari limejengwa, kuingiza mvuto wangu katika kila kitu niwezacho, kuwasaidia ninyi ndugu kuzivuta nafsi hapa Tucson, sio kuanzisha mkutano mahali popote, ama sio isipokuwa iwe ni mkutano wa muungano ama chochote kile ambacho tungekusanyikia. Kamwe sikuja kuanzisha kanisa. La, bwana. Tuna mengi sana ya hayo. Kile tunachohitaji ni kuyajaza na Wakristo waliozaliwa mara ya pili. Naam, bwana.

⁶⁰ Kwa hiyo nipo hapa kuweka juhudi zangu, na kusaidia kwa kila njia niwezayo, na popote niwezapo, na kila mlango uliofunguliwa, kutoa ushuhuda wa neema iokoayo ya Bwana wetu Yesu Kristo, na kujazwa kwa Roho Wake ambaye ameniweka miaka hii yote. Sasa, mara nyingi. . .

⁶¹ Nimemwona Tony, muda mfupi uliopita, alisema, “Sina budi kuandika, Ndugu Branham, kile nilichotaka kusema.” Nami pia. Unajua kidogo unapokuwa mzee, huwazii kama vile ulivyokuwa ukiwazia.

⁶² Mtu fulani alisema, hivi majuzi, kasema, “Ndugu Branham, una umri gani?”

“Loo,” nikasema, “Nimepita ishirini na mitano.”

“Kwa kiasi gani?”

Nikasema, “Nimeipita mara ya pili.”

⁶³ Kwa hiyo, mimi si mtoto tena. Hiyo ndiyo sababu tunazipiga wei nywele zetu katikati, ndugu. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli.

⁶⁴ Vema, kila mtu anampenda Bwana? Loo, ajabu! Sasa, hebu na tuweke kando kila mzigo mdogo na kila fadhaa ndogo sasa.

⁶⁵ Nami nashangaa, kama haitasumbua mno sasa, kwa kuwa tumeketi kwa muda mrefu, kama tungeweza tu kusimama kwa muda mfupi tu kwa ajili ya maombi.

⁶⁶ Na sasa wakati mkisimama, nitasoma mlango, ama kifungu, kutoka kwenye Biblia, wakati mkisikiliza kwa makini, mkiweza. Nitasoma kutoka katika kitabu cha Ufunuo wa Yesu Kristo, kuanzia kifungu cha 14 cha mlango wa 3.

Na kwa malaika wa kanisa la... Laodikia andika; Haya ndiyo asemayo yeye aliye Amina, shahidi aliye mwaminifu na wa kweli, mwanzo wa kuumba kwa Mungu.

Nayajua matendo yako... hu baridi wala moto; ingekuwa heri kwamba ungekuwa baridi au moto.

Basi, kwa sababu una uvuguvugu... hu baridi wala moto, nitakutapika toke katika kinywa changu.

Kwa kuwa wasema, Mimi ni tajiri... nimejitajirisha... sina haja ya kitu; nawe hujui ya kuwa wewe ni mnyonge... mwenye mashaka... maskini... kipofu, na uchi.

Nakupa shauri, ununue kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa... moto... upate kuwa tajiri, na mavazi meupe upate kuvaa, aibu ya uchi wako isionekane; na dawa ya macho ya kujipaka macho yako, upate kuona.

Wote niwapendao mimi nawakemea, na kuwarudi; basi uwe na bidii, ukatubu.

Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja nami.

Yeye ashindaye nitampa kuketi... jalia kuketi pamoja nami juu ya kiti changu cha enzi, kama mimi nilivyoshinda nikaketi pamoja na Baba yangu katika kiti chake cha enzi.

Yeye aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa.

⁶⁷ Huku vichwa vyetu vimeinamishwa, na mioyo yetu, hebu tuombe.

⁶⁸ Bwana Yesu, tunakushukuru Wewe asubuhi ya leo, Mungu wetu mwenye rehema na mwema, ambaye ulimfufua tena Bwana Yesu kutoka kwa wafu, na umemwasilisha kwetu asubuhi ya leo, katika mfano wa Roho Mtakatifu, ambaye anaibembeleza mioyo yetu tupate kutembea karibu na Yeye. Ambapo, tunapooni ile siku ikikaribia kwisha, siku ya wakati karibu inafikia sasa kuingia katika Umilele. Tunakaribia ufukoni. Tunaweza kuyasikia mawimbi yenye pofu. Ee Mungu, hii ni saa ya hatari, tunavyosoma hapa, wakati huu wa mwisho wa kanisa, Laodikia, ambapo kwamba tunakaribia ufukoni. Nao utajiri na vitu vya ulimwengu huu vimeyapofusha macho ya watu. Loo, tunaomba,

Mungu, kwamba nanga yetu itaushika huo Mwamba wa miaka, na kungojea mapambazuko. Tujalie, Bwana.

⁶⁹ Ubariki mwenendo huu wa Mungu, unaoitwa tawi la Wafanyabiashara wa Full Gospel. Tunaomba ya kwamba Wewe utalibariki tawi fulani hili hapa Tucson. Jalia lipanuke mpaka hii Ramada italazimika kuzibomoa kuta hizi na kupanua hema lake, ipate kuenea Wakristo waliozaliwa mara ya pili ambao wataingia. Tujalie.

⁷⁰ Mbariki ndugu anayekuja na uamsho, akiwa na hema humu mjini. Jalia uwe ni chombo cha kusaidia kuleta nafsi kwenye makanisa haya na—na kwenye Ufalme wa Mungu.

⁷¹ Mbariki Ndugu Bethany, juu kwenye First Assembly, wakati anapoiendeleza kazi yake kuu huko juu kwa ajili ya Ufalme wa Mungu, Bwana. Jinsi tunavyoomba ya kwamba Wewe utaendelea pamoja naye na pamoja na makanisa kote nchini.

⁷² Sasa tunapokungojea Wewe, jalia Roho Mtakatifu atupe tafsiri, na kuleta muktadha wa somo, tupate nuru, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Mwaweza kuketi.

⁷³ Hivi uliwahi kutulia na kuwazia, kwa muda kidogo tu, ya kwamba huu ungeweza kuwa ndio wakati wetu wa mwisho wa kuwahi kukutana? Hivi unajua huenda kukawa na baadhi yetu hapa, kama tukirudi tena kwenye siku nyingine ya mkutano, tutakuwa, baadhi yetu, hatupo? Hatujui yatakayotendeka. Na halafu huenda huu ukawa ndio wakati wetu wa mwisho kuketi katika kundi jinsi hii, na kushiriki na kula pamoja, humu duniani.

⁷⁴ Ila kumbukeni, unakuja wakati ambapo tutakutana tena, kwenye. . . sio kwenye—sio kwenye kiamshakinywa, bali kwenye chakula cha jioni, loo, ambako ile dhifa kuu ya Mungu, na arusi ya Mwana-kondoo, na vile viti vikuu vimepangwa kutoka anga hadi anga, nao waliokombolewa wa nyakati zote wameketi pande zote mbili mezani. Huo utakuwa ni wakati mtukufu. Ninautazamia huo.

⁷⁵ Sasa, ninataka kuchukua somo asubuhi ya leo, kuwazungumzia, kwa dakika chache tu sasa. Sitawashikilia muda mrefu zaidi ya ninavyoweza. Ninataka kuzungumza. Ninayo Maandiko machache na muhtasari nilioandika hapa, ambao ningependa kuzungumzia, kwa dakika chache, juu ya somo la: *Mlango Katika Mlango*.

⁷⁶ Sasa, huu ni mkao usio wa kawaida kabisa, tunaoona asubuhi ya leo, katika somo letu la Maandiko. Si wa kawaida kwa njia nyingi. Kwa sababu, ni moja ya Maandiko ya kusikitisha mno yaliyopo katika Biblia, ni Maandiko haya hapa, kwa kuwa yanazungumza juu ya wakati huu tunaoishi. Yanazungumzia ambapo, katika wakati huu, Yesu Kristo

ametupwa nje ya kanisa Lake Mwenyewe, huku amesimama, akibisha mlangoni, akijaribu kurudi ndani. Nao utajiri na anasa za ulimwengu zimemwondosha kanisani, hata kanisa limekuwa tu ni vuguvugu. Ni picha ya kusikitisha sana, kati ya makanisa hayo mengine yote katika nyakati za kanisa.

⁷⁷ Ndio kwanza nimalizie kuzipitia kanisani mwangu. Nami ninarudi sasa, kuanzia tarehe 17, kuichukua ile Mihuri Saba.

⁷⁸ Na sasa, katika jambo hili, tunaona ya kwamba hayo makanisa mengine yote katika nyakati za kanisa yalikuwa yamekubali. Ila ule wakati wa mwisho wa kanisa, Laodikia, Kristo alikuwa ameondolewa kwa watu. Nao walikuwa wamemweka nje ya kanisa, na Yeye alikuwa akijaribu kurudi, baada ya kutolewa nje, akibisha mlangoni. Wakawa vipofu . . .

⁷⁹ Lisilo la kawaida sana, bali, mnajua, wakati mwingine ni katika mambo yasiyo ya kawaida ambapo Mungu hutokea. Mungu hutokea katika mambo yasiyo ya kawaida kwa sababu Mungu si wa kawaida. Yeye hufanya mambo yasiyo ya kawaida. Hutokea katika nyakati zisizo za kawaida. Naye huonekana katika nyakati zisizo za kawaida, kwenye nyakati usizowazia ungeweza, Yeye angekuwa pale, hata hivyo Yupo. Lisilo la kawaida sana. “Yeye hutenda kazi kwa njia za kisiri,” Biblia ilisema, “Kufanya maaajabu yake.” Kwa hiyo, hilo linamfanya asiye wa kawaida.

⁸⁰ Na hiyo ndiyo njia. Tunaingia katika mwelekeo wa kawaida wa mambo, ndipo tunamkosa Mungu. Mambo yasiyo ya kawaida ndiyo humleta Mungu mara nyingi, mambo yasiyo ya kawaida. Jambo fulani, tunafungwa sana kwenye kanuni fulani ya imani, ama kitu fulani tunachojaribu kutumikia. Halafu basi kama kila kitu hakiji kulingana tu na vile tunavyowazia kinapaswa kuja, basi tuna—tunakiacha. “Si—Si—Si cha Mungu.” Tunafanya kosa kubwa mno.

⁸¹ Mungu hujionyesha Mwenyewe, kisha anajificha Mwenyewe katika kitu hicho ambacho anajionyesha Mwenyewe kwake. Mnaona? Yeye atajionyesha Mwenyewe katika kitu fulani, kisha anajiondoa na kujificha.

⁸² Kama vile mbegu, Yeye hujionyesha Mwenyewe katika ua la kupendeza, kisha analiacha lioze. Lakini Yeye anajificha Mwenyewe, kusudi ajitokeze tena. Naye Mungu hulifanya jinsi hiyo. Yeye ni asiye wa kawaida kabisa, nyakati zisizo za kawaida, njia zisizo za kawaida, na, wakati mwingine, vitu vidogo.

⁸³ Tu—tu—tunakosa kumpata Mungu mara nyingi kwa sababu ni, tunafikiri, ni dogo sana.

⁸⁴ Nilikuwa nikiwazia hilo dakika chache zilizopita, wakati tulipokuwa tukizungumza juu ya udogo wa tawi hili, ama vile tulivyokuwa na kundi dogo. Sasa, imekuwa ni majaliwa yangu kuzungumzia umati mkubwa. Bombay, India, nilikuwa na elfu mia tano, mkutano mmoja. Afrika, Afrika Kusini, yapata, labda

mia mbili hamsini elfu kwenye mkutano mmoja. Ila mahali ambapo nimewapata walio watamu mno na waliobarikiwa kuliko wote, ilikuwa ni wakati tulipokuwa na mikutano midogo ya nyumbani. Mungu yuko katika mahali pasipo pa kawaida na katika mambo yasiyo ya kawaida.

⁸⁵ Inanikumbusha, kwa kuwa Mkanada huyu hapa alikuwa akizungumza muda mfupi uliopita, kuhusu rafiki zangu wazuri kutoka Kanada. Wakati fulani uliopita Mfalme George ambaye nilikuwa na majaliwa ya kumwombea, kama mjuavyo, aliyekuwa na kushupaa kwa mishipa. Bwana alimponya. Ndipo akaja Kanada wakati alipokuwa bado anaugua kushupaa kwa mishipa. Naye alikuwa ni mtu hodari. Basi shule zote zikajitokeza wakati aliposhuka kupitia Vancouver, ili kwamba—kwamba waweze kutoka na kuchukua ninii yao... Wawape bendera ndogo, ya Uingereza, na—na—na kuipeperusha, kumtolea Mfalme heshima, taji, wakati akipita.

⁸⁶ Basi rafiki yangu mwema, Ndugu Ern Baxter, wakati tulipokuwa tukisikiliza kwenye matangazo wakati ikipita, yeye na malkia wake mpendwa wameketi pale. Nasi tulikuwa tumeketi chumbani, nami kamwe sitasahau hilo. Ern alishikwa sana na mhemuko hata akaruka juu kutoka kitini akanikumbatia, akaanza kulia. Nami nikasema, “Msisimko huo wote ni wa nini, Ndugu Baxter?”

Akasema, “Ndugu Branham, huyo ni mfalme wangu.”

⁸⁷ Nikawazia, “Kama inaweza kumfanya Mkanada ajisikie hivyo, kujua mfalme wake anapita, inapaswa kulifanyia nini Kanisa lililozaliwa mara ya pili, wakati Yesu akipita?”

⁸⁸ Hapo, hata hivyo, akiwa ameshupaa mishipa yake, aliketi kwenye kibandawazi chake, gari lake, na kuketi wima, ingawa alisema alikuwa akiumwa vibaya sana na vidonda vya tumboni, na mgongo wake ukimsumbua sana.

⁸⁹ Basi walimu wakawatoa nje jamaa wote wadogo, waende wakazipeperushe bendera hizi. Ndipo baada ya gwa—gwaride kwisha, mbona, watoto walipaswa kurudi shuleni. Na waliporudi, katika shule fulani, wote walirudi ila msichana mmoja mdogo. Basi mwalimu akashtuka sana wakati alipoita majina na msichana huyo mdogo hakuwako. Kwa hiyo akasema, “Sina budi kwenda kumtafuta,” naye a—akawachukua watoto. Nao wakaenda mitaani, wakimtafuta mtoto huyu mdogo. Ndipo baada ya kitambo kidogo, mwalimu mwenyewe akampata jamaa huyo mdogo, amesimama karibu na nguzo ya simu, akilia kwa moyo wake wote.

⁹⁰ Ndipo alipokuwa akilia, basi mwalimu akasema, “Kuna nini, kipenzi?” Kasema, “Hivi hukuweza kuipeperusha bendera yako kwa mfalme?”

Akasema, “Ndiyo, nilimpeperushia mfalme bendera yangu.”

Akasema, “Ulipata kumwona mfalme?”

“Ndiyo, ni—ni—nilimwona mfalme.”

“Vema,” kasema, “basi kwa nini unalia?”

⁹¹ Akasema, “Unajua, mimi ni mdogo sana. Nilimwona mfalme, bali yeye hakuniona.”

⁹² Sasa, hilo huenda likawa ni kweli, kwa Mfalme George ama mfalme mwingine yeyote, bali sivyo kwa Mfalme Yesu. Haijalishi amekupa kusanyiko dogo jinsi gani kulichunga; jinsi kazi hiyo inavyoonekana ndogo, kuzungumza tu na muuza maziwa majumbani ama mvulana muuza gazeti; Yeye ataiona. Huwezi kufanya lolote kwa ajili ya Yesu pasipo Yeye kujua. Huna budi kukumbuka, Yeye anajua kila jambo dogo ufanyalo, naye atakupa sifa yote, kwa kuwa hayo ndiyo umeamriwa kufanya. Haijalishi ni dogo vipi, lifanye, kwa vyovyote vile. Kama unataka kuipeperusha bendera yako ndogo, ipeperushe. Yeye yuko katika jambo hilo lisilo la kawaida. Huenda akamshawishi mtu.

⁹³ Ninaamini ilikuwa ni Dwight Moody. Ama nimekosea? Huenda siye. Dada mmoja mkongwe alikuwa na mzungu moyoni mwake, kwamba alitaka kuleta nafsi kwa Kristo. Naye alikuwa ni mwanamke mfua nguo. Imekuwa ni miaka mia moja na hamsini iliyopita, nadhani. Basi akaweka fedha zake mpaka akawa na akiba ya dola tatu. Ndipo akakodi banda la kale la farasi kwa dola moja kwa juma hilo. Ndipo akashuka kule, akalifisha yeye mwenyewe. Kisha akachukua benchi yake ya kuoshea na kuifanya madhabahu, na akasimamisha mimbara. Na—na mapovu yangali juu ya benchi ya kuoshea. Kisha—kisha akachukua vitini akaanza kuvisambaza. Hizo zilikuwa ni siku za mwanzoni hapa Marekani. Na kila mtu angekiangalia, anakitupa chini. Ilitokea kwamba alikuwa ni Mmethodisti. Na kwa hiyo wangekitupa—wangekitupa chini.

⁹⁴ Basi Wamethodisti wakati huo walikuwa kama vile Wapentekoste wamekuwa: kundi la washupavu. Wangelala katika nyumba za shule, wakaanguka, chini ya nguvu za Mungu, nao wakawamwagia maji usoni mwao. Wala msiniambie; nimekuwa moja kwa moja katika hiyo mikutano. Mnaona? Basi kama wangiwaacha tu peke yao, badala ya kuwarudisha, wawaache tu waendele, wangukuwa Wapentekoste. Mnaona?

⁹⁵ Lakini, basi, maskini mwanamke huyu mkongwe akivisambaza vitini hivi, na, la, kila mtu angevitupa mtaani. Basi kulikuwako na ninii... Alikuwa amesimama, akilia, kwa sababu walimkataa, wakati alikuwa amejaribu sana kumleta mhudumu mjini, kufanya uamsho. Basi mhudumu alikuwa atokee usiku huo. Alikuwa akiondoka. Basi palikuwapo na maskini mvulana mdogo amevaa ninii ya baba yake... Chini huko Kusini, tunakiita “vikazia,” mwajua. Amevaa mikanda ya kuning'inizia, nywele zilizochafuka zimening'inia shingoni

mwake, akaja na kusema, “Hei, mama, kwani unasambaza nini?”

Naye akasema, “Ni kitini, kipenzi,” akasema.

“Vema,” akasema, “siwezi kusoma.” Kasema, “Kinasema nini?”

⁹⁶ Naye akasema, “Vema, tutakuwa na mkutano huko chini kwenye banda la kale la farasi usiku wa leo.”

Akasema, “Asante. Naweza kuchukua kimoja?” akasema.

“Naam.” Naye akakiweka mfukoni mwake.

⁹⁷ Wakati mkutano ulipofanyika usiku huo, mnajua ni nani aliyekuwa kule? Mchungaji wako mwaminifu, na yule mama. Hao tu ndio waliokuwa mkutanoni. Maskini askari huyo hodari, kama kulikuwako na mmoja ama elfu moja, yeye alichukua somo lake, akasimama pale na kumhubiria mama huyo, kwa uaminifu tu jinsi angekuwa kama alikuwa akiwahubiria elfu kumi. Ni nani aliyeyumbayumba mlangoni, karibu mwanzoni mwa mahubiri, ila maskini mvulana huyu mwenye nywele zilizochafuka. Usiku huo akajikuta madhabahuni. Kama sijakosea, huyo alikuwa ni maskini Dwight Moody, aliyewatuma watu nusu milioni kwa Kristo. Mnaona? Loo, jamani! Ni mikutano mingapi na vitu vyenye madoido vilivyokuwa vikiendelea! Mnaona?

⁹⁸ Mungu yuko kwenye mambo yasiyo ya kawaida. Mungu huonekana asiye wa kawaida. Mnapaswa kukumbuka hilo.

⁹⁹ Sasa, siwezi kumkumbuka mwanasanaa aliyeichora picha hii, ya Yesu akibisha mlangoni. Ni mwanasanaa fulani wa Kiyunani. Siwezi tu kulikumbuka jina la mtu huyo wakati huu. Lakini alikuwa ametumia karibu maisha yake yote, akiichora picha hii. Basi, mnaona, kabla haijatundikwa katika ukumbi wa umaarufu, haina budi kupitia kwenye ukumbi wa wakosoaji kwanza. Picha yoyote kuu haina budi kufanya hivyo. Haina budi kukabiliana na wakosoaji.

¹⁰⁰ Loo, laiti ningalikuwa na ki—kitu kinachohitajika kulitupia hilo mbele ya kusanyiko hili asubuhi ya leo. Hivi mnatambua, enyi Wapentekoste, wakati tunapopoa, kwamba Mungu ametupitisha kwenye ukumbi wa wakosoaji siku hizi? Kanisa halina budi kupitia kwenye ukumbi ya wakosoaji kabla halijaingia katika ukumbi wa umaarufu, kama Bibi-arusi. Hakika. Mnaweza kuvumilia hilo? Mko tayari kujitokeza na Maandiko, na kusimama kishujaa kwa ushuhuda wenu katika upendo wa Kristo? Unarudisha, unatoka nje na ulimwengu? Kama vile Biblia ilivyosema, “Demasi ameniacha, akiupenda huu ulimwengu wa sasa.” Hapo ndipo kanisa linaposimama leo hii, limewekwa kwenye mizani. Hiyo ndiyo sababu, linakuwa Laodikia.

¹⁰¹ Picha hii, kama vile yule mwanasanaa alivyoichora, wakati ilipopelekwa kwenye ukumbi wa wakosoaji wasingeweza kuona

kasoro yoyote. Basi hatimaye mkosoaji mkuu akaja, naye akasema, “Kuna kasoro moja kwenye picha yako.” Akasema, “Ni kweli, Yesu akiwa na taa ya kandili mkononi Mwake, akija usiku katika giza la dhambi. Hiyo ni picha nzuri. Sura yake pamoja na matumaini ya mtu fulani kuja mlangoni wakati Yeye akibisha,” kasema, “hilo ni zuri sana. Na mtazamo juu ya uso Wake, wakati akitamani kusikia kutoka huko ndani. Ila, bwana, hakuna komeo mlangoni. Kama angalikuja, Yesu angewezaje kuingia, kwa sababu hakuna komeo mlangoni?”

¹⁰² “Loo,” kasema mwanasanaa, “Niliichora jinsi hiyo, kwa kuwa komeo liko upande wa ndani. Yesu hawezi kuingia tu kwa mapenzi Yake. Inabidi iwe ni mapenzi yako kumkaribisha ndani.”

¹⁰³ “Tazama, nasimama mlangoni nabisha. Mtu yeyote akiisikia Sauti Yangu, na kuingia... kunifungulia, nitaingia na kula pamoja naye, na yeye pamoja Nami.”

¹⁰⁴ Hiyo ndiyo picha tunayoangalia sasa. Mtu hubisha mlangoni kwa nini? Ni kitu gani kinachomfanya mtu kubisha mlangoni? Anajaribu kupata njia ya kuingia. Anajaribu kuingia ndani. Kuna... Labda kuna jambo analotaka kukuzungumzia kulihusu, ama labda anataka kuzungumza nawe juu ya biashara fulani ama kitu fulani. Ama—ama, labda anataka kukupa kitu fulani. Kuna sababu fulani, la siyvo asingekuwa akibisha mlangoni. [Ndugu Branham anagongagonga mimbarani—Mh.] Mnaona? Tungeninii tu... Heshima ya kibinadamu ingekuwa tu ni kuufungua mlango na kuona anachotaka mtu huyo. Hilo ndilo tu jambo la kibinadamu kufanya: kufungua mlango, kumuuliza huyo mtu, “U nani wewe? Wataka nini?”

¹⁰⁵ Anataka, labda, anataka kukutembelea, kuketi tu chini, kusema, “Mimi ni rafiki yako. Ningetaka kuzungumza na wewe kidogo tu asubuhi ya leo.” Kisha aketi, kama ni rafiki, uzungumze naye. Kama ni mtu anayetaka kitu fulani kutoka kwako, mngeweza kulizungumzia. Mnaona?

¹⁰⁶ Watu wengi mashuhuri wamebisha milangoni, kote katika maisha. Sasa, mengi sana yake yanategemea, ukiisha kufika mlangoni, ni nani anayebisha. Inakupasa kujua ni nani huyo anayebisha. Lakini inakupasa, angalau, kwenda mlangoni. Hilo tu ndilo jambo la heshima kufanya, ni kujua ni nani aliye hapo mlangoni. Nenda pale, kama mtu fulani anabisha, useme, “Ni nani?” Fungua mlango. “U nani wewe? Unataka nini?” Loo, wengi—wengi, huenda ikawa ni mtu fulani mashuhuri. Vipi kama ni mtu mashuhuri? Ingekuwa ni heshima kubwa kwako, kama ulimfungulia mlango mtu ambaye ni mashuhuri.

¹⁰⁷ Unafikiri ingekuwaje, miaka michache iliyopita, wakati Adolf Hitler alipokuwa Kiongozi wa Ujerumani? Unafikiri nini juu ya maskini jamaa anayeishi huko chini kichochoroni, ama huko chini mtaani mahali fulani, kama angalisikia

mbisho mlangoni asubuhi moja, mwajua. [Ndugu Branham anagongagonga mimbarani—Mh.] Naye akaenda mlangoni, naye maskini mtumishi huyu wa Kijerumani amesimama pale, na pale alisimama Adolf Hitler amesimama mlangoni? Mbona, alikuwa ndiye mtu mkuu kuliko wote Ujerumani wakati mmoja. Mnaona? Hakika. Mbona, alikuwa ni mtu mashuhuri.

¹⁰⁸ Mnajua yale maskini mtumishi huyo angefanya? Nusura azimie. Angelisimama sawasawa, apige saluti yake ya Kijerumani, aseme, “Kiongozi mkuu wa Ujerumani, ingia nyumba yangu duni. Chochote hapa unachotamani, lolote ambalo mtumishi wako anaweza kufanya, nijulishe tu. Nitalifanya kwa furaha.” Loo, ni heshima jinsi gani!

¹⁰⁹ Mnajua nini? Kila gazeti Ujerumani lingaliandika makala hiyo, ya Adolf Hitler mkuu akishuka kwenda kwa nyumba ya askari wa kawaida, na kubisha mlangoni na kuomba kitu fulani. Kwamba Hitler angemwomba mtumishi kitu fulani, angekuja nyumbani mwake, na—na kuiheshimu nyumba yake, vema, hilo lingekuwa ni jambo kuu jinsi gani! Ninii, na ninii . . .

¹¹⁰ Kama ungalikuwa huko Italia, na katika siku za Mussolini. Naye Mussolini alikuwa ni dikteta wa—wa—wa Urumi, Italia. Basi vipi kama mtu fulani maskini huko chini mtaani angalisikia mbisho mlangoni asubuhi fulani? [Ndugu Branham anagongagonga mimbarani—Mh.] Na pale alisimama Mussolini mlangoni. Loo, jamani! Mioyo yao ingalitetemeka, “Vema, dikteta mkuu, mheshimiwa bwana mkubwa, ingia nyumbani mwangu.” Akitetemeka na kuhangaika, “Ni—nifanyeje? Kuna chochote hapa ambacho—ambacho ungetaka? Kuna jambo fulani mtumishi wako analoweza kukufanyia?” Loo, ingekuwa ni heshima kubwa kwa Mrumi yeyote kumpokea Mussolini nyumbani mwake.

¹¹¹ Ama vipi ikiwa malkia wa Uingereza, leo hii, angekuja hapa Tucson, na kushuka hapa kwenye uwanja wa ndege, naye angekuja kwenye moja ya nyumba zetu hapa? Moja ya ninii zetu . . . Sisi ni watu wa kawaida tu. Na kama malkia wa Uingereza angekuja kutoka Uingereza, kote kupita bahari, ashuke hapa nje kwenye uwanja wa ndege, kwenye—kwenye uwanja wa ndege naye angeletwa na teksi, na aje na kuubisha mlango wako. [Ndugu Branham anagongagonga mimbarani—Mh.] Nawe, mama wa heshima ama mwanamume muungwana, ungeenda mlangoni na kusema, “U hali gani?” Naye huyo hapo amesimama pale, kama tu mwanamke wa kawaida. Nawe ungesema, “U hali gani? U nani wewe?”

¹¹² “Mimi ni malkia wa Uingereza,” naye angejitambulisha. Loo, jamani, ni heshima ya jinsi gani! Ni upendeleo wa jinsi gani!

¹¹³ Kila gazeti kote Tucson, kote Marekani, ingekuwa kwenye habari za kitaifa, kwamba malkia mkuu wa Uingereza alikuja

kote hadi Tucson, Arizona, akakutembelea, mtu maskini. Hadhi ambayo ingeongezea kwa malkia, kujinyenyekeza kuja mlangoni pangu ama mlangoni pako. Vema, unajua kile angesema? Ingawa yeye si... Wewe huko chini ya himaya yake, bali hata hivyo yeye ni mtu mashuhuri. Yeye ndiye malkia aliye mkuu kuliko wote ulimwenguni. Inapofikia mambo ya kitaifa, yeye ndiye malkia wa taifa aliye mkuu kuliko wote ulimwenguni. Mbona, ungesema, "Mheshimiwa malkia, ingia nyumbani kwangu. Endapo kuna chochote hapa ambacho ungetaka kuchukua, lolote unalotaka kufanya, jisikie tu umekaribishwa." Mbona, hakika. Nayo magazeti yote yangeiandika.

¹¹⁴ Ama hata asubuhi ya leo, iwapo rais wetu, Kennedy, angekuja mlangoni pako. Loo, huenda usikubaliane naye, juu ya siasa, bali hata hivyo ungemruhusu aingie. Kwa nini? Si kwa sababu labda yeye ni mtu tu, bali ni kwa sababu yeye ni nani. Yeye ni rais wa Marekani yetu. Hata hivyo, tungeninii, huenda tusikubaliane naye (nisingekubaliana naye) katika siasa. Lakini, hata hivyo, ungeheshimika kutembelewa na Rais Kennedy mlangoni pako.

¹¹⁵ Vipi kama alifanya ziara maalum kuja mlangoni pako? Mbona, ingekuwa kwenye habari kila mahali: "Bw. Kennedy mnyenyekevu, rais wa Marekani, aliruka kwa ndege hadi Tucson, Arizona, kuja mlangoni pa John Doe." Ingekuwa ni heshima kuu jinsi gani kwake, na ni heshima jinsi gani kwako. Mbona, kwa vyovyote vile usingemfukuza. La hasha. Hakika ungempokea, maana yeye ni mtu mashuhuri.

¹¹⁶ Lakini ni nani aliye mkuu kuliko Yesu? Naye anafukuzwa kutoka kwenye milango mingi kuliko madikteta wote na wafalme na watawala wa ulimwengu. Naam. "Ninasimama mlangoni nabisha; na kama mtu yeyote ataisikia Sauti Yangu na kuufungua mlango, nitaingia na kula pamoja na yeye."

¹¹⁷ Loo, mibisho hii midogo tunayopata mlangoni. Mara nyingi, Yesu hubisha mlangoni mwa moyo wetu. Hapo ndipo kanisa lilipo leo hii. Mibisho hiyo midogo, unaihisi, hapana shaka, sasa hivi. Ni kitu gani? Ni Yesu, akijaribu kuingia, apate namna ya kuingia kwenye mlango wa moyo wako. Ana ninii... anataka kuzungumza nawe kidogo.

¹¹⁸ Na kama ungemheshimu rais, vipi kuhusu Yesu? Kama wewe, kwa vyovyote vile, usingeweza kumkataa rais, ungewezaje basi kumkataa Yesu? Rais ni mwanadamu tu; hana budi kufa. Lakini Yesu ni Mungu wako. Yeye ni Hakimu wako. Si hilo tu, bali yuyo Huyu, ndiye Hakimu wako, sasa ni Mwokozi wako.

¹¹⁹ Sasa, huenda rais anataka kukuamrisha kwenda Jeshini. Henda akakuita ku—kufanya jambo fulani ambalo lingekuwa ni baya sana kufanya. Huenda akakuita, ama kuchukua kitu fulani kutoka kwako, awachukue watoto wako ama kitu fulani,

wawe watumishi wake ama kitu fulani. Huenda akafanya jambo kama hilo.

¹²⁰ Bali Yesu hataki hilo. Anataka kukupa kitu fulani. Hiyo ndiyo sababu Yeye anabisha. Anacho kitu fulani kwa ajili yako. Hakuna kitu ambacho kingeweza kuwa kikubwa kuliko kile anachotaka kukupa: Roho Mtakatifu. Anataka kukupa Uzima wa Milele.

¹²¹ Vipi kama rais angesema, “Nitafanya...Ninakuja kukuchukua, nami nina mamlaka ya kufanya hivyo, na kukufanya rais wa Marekani”? I—itakubidi kuuacha wakati fulani. Vipi kama malkia alitaka kukufanya malkia wa Uingereza, nawe uvae taji? Hiyo, itakubidi kuiacha.

¹²² Lakini Yesu anatupa taji ya Uzima, ambayo hatuiachi, taji isiyoharibika ya Utukufu Wake. Wala haitatubidi kuiacha Hiyo. Yeye hutupa Hiyo. Ni baraka. Ni Roho Mtakatifu, ambaye anataka kuyatia taji maisha yetu kwake.

¹²³ Tungewezaje kuwa wasiojali hivi, kuikataa? Ni mambo ya kipumbavu jinsi gani ambayo kanisa hufanya! Jinsi watu wanavyoweza kuwa na pupa, kufanya kosa kama hilo, kukataa kusikiliza mbisho huo mlangoni. [Ndugu Branham anagongagonga mimbarani—Mh.] Jinsi—jinsi ingekuwa ni kichaa kwa mwanamume ama mwanamke yeyote, aliyepo asubuhi ya leo, kuuondokea mbisho huo, Uzima wa Milele!

¹²⁴ Nasi tunaangalia na kuona mawingu ya hukumu yakiingia, kuisikia sayansi ikisema, “Ni dakika tatu ifike usiku wa manane.” Na kwa kweli dakika mbili za hizo zimekwisha. Hiyo ilikuwa ni miaka kadhaa iliyopita.

¹²⁵ Nasi tunaona kanisa limetawanyika. Tunaona kila kitu kikiendelea, jinsi kinavyoendelea, nayo madhehebu yanaaza kuwa madhehebu, kule kupoa. Nazo siku za uamsho karibu, inaonekana kwamba, zimekwisha. Afadhali tukabiliane na ukweli. Loo, tuna kelele nyingi sana, hakika, kupiga piano, kuruka-ruka juu chini. Wanawake wanakata nywele zao, na macho ya samawati, na kupiga makelele, na wanaume wakiwaruhusu kufanya hivyo! Hayo ni kinyume na Maandiko.

¹²⁶ Tamasha ya kuchukiza jinsi hiyo kama tunavyoona mitaani mwetu siku hizi! Niliwachukua watoto wangu jana, walitaka kushuka wakaone gwaride la farasi likipita; watoto wangu wadogo. Baba yangu alikuwa mpanda farasi hodari, na mimi—mimi nimewapanda kidogo, basi kuko tu ndani yao kuwapenda farasi. Nao walitaka kuwaona hao farasi. Basi niliposimama mtaani, nikawa mgonjwa ndani yangu kabisa kisha nikarudi, kuona jinsi, watu siku hizi, wanavyojaribu kuishi katika siku za nyuma, wakijaribu kuishi kitu fulani kilichokuwako.

¹²⁷ Tuko katika ulimwengu unaobadilika. Daima unabadilika, nchini mwangu. Mimi ni Mkentakiki, mwajua, kwa kuzaliwa. Hiyo ni kusema, watu wangu wote wanaishi kule, karibu

wote. Nao wana Bonde la Renfro. Wanajaribu kuiga watu wa milimani, na—na kuwasha taa za mafuta, na—na kupika kwa—kwa jiko la kuni, na kuvaa nguo kama wa—watu wa mipakani wa mwanzoni walivyovalia. Wako—wako kwenye ulimwengu unaobadilika, wakijaribu ku—ku—kuishi katika ninii—katika ninii... Mko katika wakati wa kisasa, mkijaribu kurudi na kuishia kitu tofauti kilichokuwapo. Ni kitu gani kinachomfanya mtu kufanya hivyo? Kwa sababu yeye anapaswa kufanya hivyo.

¹²⁸ Lakini basi unajaribu kuwaletea Injili isiyobadilika, hawaitaki hiyo. Wanataka kitu fulani cha kisasa na mamboleo, mtu fulani atakayewapapasa mgongoni na kuwaacha waendeleo kwa kujiunga tu na kanisa, huku wakiishi vyovyote watakavyo. Lakini inapofikia kwenye kuirudia Injili kweli, hawaitaki. Na kitu hicho hicho ndani yao kinachoona njaa ya kurudi, ni Injili. Nao wanajaribu kukiridhisha kwa kuvirudisha vitu vya kawaida, huku wakivikataa vitu vya kiroho. Mnaona jinsi Ibilisi anavyoibadilisha I—Injili kwa watu?

¹²⁹ Sio kuwadharau dada zangu, lakini kama, katika siku za mwanzoni, mwanamke angekuja mjini kama nilivyowaona wengine jana, amevaa jozi ya suruali ndefu! Jinsi huyo mama alivyoingia ndani ya hizo, ilionekana tu kana kwamba ngozi ilikuwa upande wa nje. Sijui jinsi huyo mwanamke alivyoingiza mguu wake ndani yake. Akitembea mtaani huko chini! Wakati, Biblia ilisema, “Mwanamke atakayevaa vazi limpasalo mwanamume ni chukizo machoni pa Mungu.”

¹³⁰ Na pamoja na hiyo samawati, yote nyuma ya macho yake, kama angalipitia kwenye mji wa mpakani, daktari wa kale angalimlaza hospitalini, na kuuweka huo mji katika karantini, kwa ugonjwa, kwamba, “Mwanamke alioza kabla hajafa.” Hiyo ni kweli. Ugonjwa wa jinsi hiyo!

¹³¹ Kisha unajaribu kurudi nyuma na kuishi jambo fulani, halafu unakataa mbisho wa Injili ya mtindo wa kale ya Roho Mtakatifu, na kama ilivyokuwa katika Siku ya Pentekoste pamoja na sifa zile zile iliyokuwa nazo ndani yake, kutusafisha na kutufanya viumbe vipya. Tunaishi katika vivuli, nalo kanisa liko katika wakati huo wa Laodikia, “Tajiri, hawana haja na kitu.” Sasa, sisi Wapentekoste hatuwezi kuwapigia makelele sana Wabaptisti na Wamethodisti, maana chungu hakiwezi kuiita birika nyeusi, mwajua. Kwa hiyo tumefanya jambo lile lile. Sasa, hiyo ni kweli.

¹³² “Basi, tazama, nasimama mlangoni nabisha, mtu yeyote...” Sasa, kumbukeni, Biblia ilisema Yeye alikuwa nje ya kanisa, katika wakati huu, akijaribu kuingia. Sasa, huwezi kulikanusha Neno la Mungu. Unaona? Alikuwa akijaribu kuingia, akisihi aingie ndani. “Mtu yeyote atakayeufungua mlango, aniruhusu niingie, loo, nitaingia na kula pamoja naye.” Mnaona? Yeye analo jambo analotaka kuzungumza na wewe, shughuli fulani, ama

mpango wa wokovu. Anataka kuzungumza na wewe. Lakini labda mmezama sana katika kanuni za imani mkawa wagumu sana, wasiojali, hata hamtaki kumsikia akizungumza. Hiyo ni kweli. “Tazama, nasimama kwenye. . .”

¹³³ Unasema, “Loo, Ndugu Branham, sasa hebu kidogo tu. Tayari nimemruhusu kuingia.” Vema, labda ulifanya hivyo hasa. Lakini labda hayo tu ndiyo uliyofanya, kumwacha tu aingie. Unaona, watu wengi hawaninii. . . Wanaogopa mawazo yenyewe ya kuzimu, nao wanajua wanaelekea huko pasipo na Kristo. Mnaona? Nao watasema, “Vema, nilimkaribisha ndani, hakika, miaka thelathini iliyopita, miaka ishirini iliyopita.” Lakini huenda ikawa hilo tu ndilo ulilofanya.

¹³⁴ Vipi kama nikija nyumbani mwako, na kubisha mlangoni, useme, “Karibu ndani, Ndugu Branham”? Niingie. “Lakini wewe simama papa hapa. Usiende kuchunguza-chunguza kila mahali, kupekuapekua kote nyumbani mwangu.” Unaona?

¹³⁵ Sasa, hivi mnajua, ndani ya mlango wa moyo wa mwanadamu tuna vyumba vidogovidogo vya siri? Loo, hatutaki kulikubali, bali ni kweli. Hakika, tuna vyumba vidogovidogo vya siri. Naam, bwana. Tunapenda kuita. . . Tunamkaribisha, moyoni mwetu, bali hatutaki kumfanya Yeye Bwana wetu. Hatutaki kwenda kuzimuni, kwa hiyo, “Yesu, Wewe ingia mlangoni, kusudi nisiende kuzimuni, ila huwezi kuwa Bwana wangu.”

¹³⁶ Sasa, *Bwana*, ni “umilikaji.” Hilo linamaanisha, unapomkaribisha ndani kama Bwana, Yeye anatawala kila kitu. Yuko nyumbani.

¹³⁷ Ninapokuja nyumbani kwako na kubisha mlangoni, iwapo hunitaki, useme, “Toka mlangoni pangu,” ningekuthamini zaidi. Kama ungeniruhusu niingie mlangoni, useme, “Sasa usiende ukipekuapekua huku na huku. Simama papo *hapo*. Sasa, unataka nini?” Unaona? Ningejisikia kukaribishwa? Ningeweza kuelezea matembezi yangu kwako? La hashu.

¹³⁸ Na hivyo ndivyo kanisa lilivyo leo hii, rafiki. Hivyo ndivyo watu wanavyokuwa. “Karibu ndani, Bwana, lakini sasa, ni, ni hayo tu. Niambie unachotaka.” Unaona? Loo, la. Hapo—hapo ndipo tunapoingia matatani.

¹³⁹ Hatuna budi kumkaribisha: “Bwana, karibu nyumbani mwangu. Kama kuna chochote, kama kuna chochote humu ndani unachotaka, karibu. Mimi ni Wako. Wewe ni wangu. Umeniheshimu. Mfalme mkuu, Muumba wa mbingu na nchi, amebisha mlangoni pangu. Nami ninataka uingie, Bwana. Bwana, kuwa Bwana wangu. Nichukue. Nifanyie lolote utakalo. Kitu chochote kibaya kilicho ndani yangu, fichua kila siri iliyoko moyoni mwangu. Ingia kwenye kila mlango. Nichunguze kabisa, Bwana, uone nina ubaya gani. Na chochote kibaya, unionyeshe, Bwana. Kitupe nje ya mlango. Ninakutaka Wewe humu ndani.

Nilikukaribisha ndani, kuwa Bwana wangu. Sina baraka hiyo, Bwana. Nisafishe sasa.”

¹⁴⁰ Ikiwa siwezi kumfanya Bwana wangu mkamilifu, kamwe sitamfungulia mlango, ikiwa hawezi kuwa Bwana. Sitaki tu awe Mwokozi, iwapo hawezi kuwa Bwana. Ikiwa mimi. . . Kila mtu anataka Mwokozi, bali hawamtaki Bwana. Wanataka kitu fulani, ambacho wanaweza kuitoroka hukumu yote ya kuzimu, halafu wanaweza kuishi vyovyote wanavyotaka kuishi, wafanye wanalotaka kufanya.

¹⁴¹ Mwajua, hebu tuzunguke tu kwenye jengo la moyo. Mtanivumilia dakika zingine kumi? Tazameni. Angalieni. Hebu tuuzunguke moyo kwa dakika moja.

¹⁴² Kitu cha kwanza, unapoingia kwenye moyo wa binadamu, upande wa kulia unapoingia, upo mlango mdogo pale, nao unaitwa “maisha yangu ya binafsi.” Sasa, hutaki mtu kujipumbaza katika huo. “Sasa, kama nikitaka kufanya lolote, hiyo ni shughuli yangu. Nitajiunga na kanisa, nami nitashuka kule. Lakini, mhubiri, usiniambie ninayopaswa kufanya.” Loo, naam. Mnaona? “Sasa, ninajua Biblia inasema Hilo, bali siliamini Hilo.” Loo, jamani! Mnaona? Halafu, unafikiri Yesu angekaa ndani ya moyo kama huo? Hakika hawezi. Yeye huingia apate kuwa Bwana. Yeye huingia, Yeye ambaye. . .

¹⁴³ Na hayo—hayo maisha ya binafsi, loo, hilo ni jambo kuu. Sasa, mnajua tunataka maisha yetu wenyewe ya kibinafsi. “Kama tukitaka kinywaji cha kijamii pamoja na jirani yetu, hiyo ni shughuli yetu. Kama sisi wanawake tungetaka kuzikata nywele zetu, hilo ndilo. . . Hiyo ni fursa yetu wenyewe ya Marekani. Kama tunataka kuvaa kaptura, hiyo ni shughuli yetu.” Vema, hiyo ni kweli. “Kama sisi wanaume tunataka kunywa kileo cha kijamii, na kama tunataka kuwaruhusu mke wetu kufanya hivyo, huna shughuli yoyote kusema neno moja kwetu.”

¹⁴⁴ Lakini Injili ilisema, “Msifanye hivyo.” Sasa, ni neno la nani lililo kweli? Mnaona? Neno la Mungu ni la kweli.

¹⁴⁵ Mnasema, “Loo, hakika, tunataka—tunamtaka Yesu.” Hakika. Tunafikiri tunaye, na yote namna hiyo.

¹⁴⁶ Lakini nashangaa kama huo Unyakuo ungeweza kupita, nasi tuachwe peke yetu siku moja, ndipo tushangae wote uko wapi, kama ungalikuja kisiri sana, mwajua. Na hivyo ndivyo unavyokuja, kama mwizi usiku. Mtaninii. . . Tisini na tisa kutoka kila nusu milioni, kila milioni, kamwe hawatajua Unyakuo umetukia. Utakwisha wala hata hawatajua kitu kuuhusu. Yesu alisema hivyo. Kwa hiyo hilo linaifanya kweli. Mnaona? Hakika. Utakuja kama mwizi usiku, na waibwe waende.

147 Kama kitabu kile nilichosoma wakati mmoja. Jamaa huyo alikuwa ni nani? Romeo na Juliet, ama kitu kama hicho, mnaona, alikuja akamchukua msichana usiku.

148 Hivyo ndivyo Yesu anavyofanya. Wakati ulimwengu umelala tu kivivu katika usingizi, kama vile Biblia ilivyosema, wakati wa Laodikia, Yeye atanyemelea amchukue huyo Bibi-arusi. Halafu, wote wale waliofufuka, kote katika nyakati, waliokuwa kote katika nyakati, wote wataenda Mbinguni katika Bibi-arusi.

149 Ndipo hukumu itakuja. Kanisa litasema, “Vema, ngoja kidogo. Nilifikiri kulipaswa kuwapo na Bibi-arusi, Kuja kwa Bwana na Bibi-arusi.”

150 “Kumekwisha muda mrefu uliopita.” Mnaona? “Hamkujua lolote juu yake.” Mnaona? “Kulitokea kisiri.”

151 Kwa nini? Tunasema, “Loo, mimi ni mfuasi wa kanisa. Mimi ni Mmethodisti. Mimi ni Mbaptisti. Mimi ni Mpentekoste.” Hilo halimaanishi hata kitu kimoja kwa Mungu.

152 Si zaidi ya daktari kusema, “Una kansa, iko kwenye kiwango cha juu.” Na hilo—hilo halina uhusiano wowote na ugonjwa huo. Hilo ni kuupa tu jina. Ni ibilisi, mnaona, “kansa.” Kama ungesema, “Yule ni hua. Yule ni mwewe. Yule ni namna fulani ya koho.” Hilo—hilo—hilo halina uhusiano wowote, kile. . . Pia, mnaona, hilo haliutibu. Hilo haliuui. Linasema tu kile ulicho.

153 Kusema tu, unasema, “Mimi ni—mimi ni Mkristo. Mimi ni. . .” Kwa kukiri tu, labda. Mnaona, ma—maisha yetu yananena kwa sauti kubwa sana hata ushuhuda wetu hausikiki; maisha yetu, matendo yetu, uadilifu wetu miongoni mwetu.

“Watakuwa na uamsho hapa.”

“Ni nani aliye nao?”

“Wabaptisti.”

154 “Ah, hatutakuwa na uhusiano wowote na huo.” Na labda Mungu ana ujumbe pale kwa ajili yetu.

“Ni nani aliye nao?”

155 “First Assembly, Second Assembly, ama ninii—ama Jina la Yesu, ama ninii—ama Church of God, ama—ama kitu fulani.”

“Loo, vema, sisi—sisi, sisi hatuko kwenye kundi hilo.”

156 Sisi ni ndugu. Mtu yeyote anaweza kuthubutu kuutenganisha urithi wa Mungu? Walimpokea Roho Mtakatifu kama ulivyompokea, wakafanya mambo yale yale uliyofanya ulipompokea. Hakika.

157 Lakini unaona ni kwa nini ninalipenda hili la Wafanyabiashara wa Full Gospel? Linaleta njia kuu, ambapo ninayaelezea mambo haya, mnaona, kusema, “Jambo ndilo Hili.” Sisi ni ndugu. “Hatujagawanyika. Sisi sote ni Mwili mmoja,” mnaona, kama alivyosema mshairi.

158 Sasa, “Huo mlango mdogo wangu binafsi, maisha yangu ya kibinafsi, sasa, hilo ni sawa. Nitakuwa mshirika wa kanisa lako. Nitajiunga na Wafanyabiashara wa Full Gospel. Lakini, sasa, usianze kuniambia inanipasa kumpokea huyu Roho Mtakatifu na kupiga makelele namna hiyo.” Mnaona? Hayo ni hayo maisha ya mtu binafsi. Mnaona? Kamwe hutaupata Utawala wa Yesu kwa kufanya hilo. Yeye atageuka tu moja kwa moja na kutoka mlangoni.

159 Ungefanya nini katika kisa kama hicho, kama mtu fulani, kama ulienda kwenye nyumba fulani, nao wakasema, “Simama hapa mlangoni. Sema unachotaka?” Vema, ungesema, “Asante,” ugeuke utoke mlangoni. Vivyo hivyo na Yesu. Hakika. Hiyo ndiyo sababu kanisa limeachwa, likiwa baridi, mnaona, jinsi tu lilivyo. Kamwe msiache Wafanyabiashara wa Full Gospel wafikie kiwango hicho.

160 Unapousikia Ujumbe, na kusikia mbisho [Ndugu Branham anagongagonga mimbarani—Mh.], fungua useme, “Bwana, Hili lote linahusu nini?” Unapomwona mtu... Tuna waigaji wengi sana. Lakini unapomwona aliye halisi!

161 Mwigaji anamaanisha nini? Dola ya bandia inamaanisha nini, unapookota dola iliyo bandia? Inamaanisha ilifanyizwa kutokana na iliyo halisi. Hapana budi pawe na iliyo halisi, kuifanya hiyo ya bandia.

162 Kwa hiyo kuna Roho Mtakatifu halisi, nguvu halisi za wokovu, Mungu halisi wa upendo. Naam. Usichukue chochote pungufu. La, bwana, usichukue. Vema. Huo mlango wa binafsi...

Itanibidi kuharakisha kupitia milango hii.

163 Kuna mlango mdogo wa majivuno, pia. Loo, jamani! Huo ni mbaya. Heri tusikae penye mlango huo muda mrefu kupita kiasi. Lakini unataka kusimama katika mlango huo wako mwenyewe, na kusema, “Sasa, usianze kuniambia chochote.” Unaona? “Mbona, ninajivunia hali yangu mwenyewe.” Hakika, bali hupaswi kufanya hivyo.

164 Nilihubiri hapa, si muda mrefu uliopita, juu ya *Mwana-Kondoo Na Hua*. Naye mwana-kondoo, mnaona, mwana-kondoo, kondoo, yeye hatoi ila kitu kimoja, hicho ni sufu. Hiyo ndiyo anayotoa. Naye husalimisha haki zake. Unaweza kumchukua kondoo na kumrusha juu, na kumfunga kwa m—mpini, namna *hiyo*, na kumnyoa manyoya yote. Yeye atalala pale tu. Huachilia haki zake. Hata hivyo, yeye ndiye aliyekuza hiyo sufu. Ni mali yake, bali anaiachilia.

165 Unapomwambia mtu ya kwamba hana budi kuzaliwa mara ya pili, hana budi kusafishwa, kutokana na maisha ya dhambi. Yeye, yeye hana budi kuacha kusema kwake uongo, kuiba, kudanganya, na—na kubadili dini, na kufanya yasiyofaa. Jamani, baadhi yao wanalipuka kama puto; sasa, mnaona, huyo

ni mbuzi, mnaona, yeye atazua ugomvi. Lakini mwana-kondoo halisi ataachilia haki zao.

¹⁶⁶ Niliwaambia kina mama wetu wakati mmoja, kuhusu... Sio kwamba nina neno dhidi ya kina mama; hao ni dada zetu. Lakini nina bidii ya Kanisa hili. Ninapoonamambo ya ulimwengu kama Sodoma yakiingia ndani yake, basi inanibidi kupaza sauti dhidi yake. Kuna kitu fulani ndani ambacho moyo wangu huugulia, na ninalia. Msijilinganishe na Marilyn Monroe ama baadhi ya hawa wanawake kule. Fanyeni kama Sara katika Biblia. Mnaona? Msijaribu kuwa Bw. Kitu Fulani, kinginecho, kukimbia jukwaani na kupiga makelele, na kujaribu kuvaa kama mtanashati fulani, na kunywa kidogo na kutojali. Msifanye hivyo. Tuna maonyesho mengi mno ya Hollywood katika Pentekoste. Hiyo ni kweli. Tunahitaji Roho Mtakatifu. Sasa, huenda msinipende, huenda msitake nirudi tena. Lakini hii ni nafasi ya kusema Kweli, na hii ndiyo Kweli. Ijaribuni, tafuteni kujua kama sivyo.

Mama fulani alisema, “Ni majaliwa yangu mwenyewe ya Kimarekani.”

Nikasema, “Lakini unaachilia hayo.”

¹⁶⁷ Wakati fulani uliopita, mimi na mke wangu tulikuwa tukienda kwenye duka la vyakula huko Indiana, ndipo tukaona jambo la kigeni, mama mmoja alikuwa amevaa sketi. Lilikuwa la kipekee sana. Akasema, “Mpenzi, hivi—hivi watu hao hawaimbi katika kwaya?”

Nikasema, “Naam. Naam.”

“Vema, kwa nini?”

¹⁶⁸ Nikasema, “Vema, unaona, mpenzi, hao, hao si wa Ufalme wetu,” kasema, nikasema, “wa Ufalme wetu.” Nikasema, “La.”

¹⁶⁹ Nimekuwa mmishenari, mara nyingi kuuzunguka ulimwengu. Ninakuta, nikienda Ujerumani, ninapata roho ya Kijerumani. Nikienda Ufini, kuna roho tofauti. Nikienda Australia, kuna roho nyingine. Nikija Marekani, kuna roho nyingine. Ni roho ya kitaifa, na hizo zote ni za ibilisi. Yesu alisema hivyo. Falme za ulimwengu huu ni za ibilisi. Yeye anatawala kila moja ya hizo. Sasa, Yesu alisema hivyo.

“Kwa hiyo, mnaona, ni roho hiyo ya kitaifa.”

“Vema,” akasema, “hivi sisi si Wamarekani?”

Nikasema, “La, bwana. Kwa uwezekano, ndivyo tulivyo.”

¹⁷⁰ Kasema, “Wewe ni nini?” Nikasema... “Vema, hivi hatupaswi kufanya kama Wamarekani?”

¹⁷¹ Nikasema, “La, sio kundi hili la ulevi, ugomvi, linalotahayarisha. La, bwana. Tumezaliwa kwa Roho wa Mbinguni. Tumetoka ambako usafi, utakatifu usioghoshiwa, ambako Malaika na haki wako mbele za Mungu.” Nikasema,

“Tunaishi hapa kama taifa, hakika. Hiyo ni kweli. Hili ndilo taifa letu, jinsi tulivyo hapa, tukijaribu. Lakini ninii yetu, ‘Ufalme Wako na uje. Mapenzi Yako yafanyike duniani, kama ilivyo Mbinguni.’”

¹⁷² Kwa hiyo, tunapozaliwa kutoka Juu, na dhambi yote imeondolewa kote kutoka kwenye lile shimo, ni Roho wa Mungu ndiye anayeingia, yule Muumba, ndani ya moyo wetu, na Yeye huendesha tabia yetu. Hatusemi uongo, kuiba, kudanganya. Waaminifu, waadilifu, tunatembea kama raia wa Mbinguni, kwa kuwa ndivyo tulivyo kama tumezaliwa kwa Roho wa Mungu.

¹⁷³ Basi wengi wetu huchanganyikiwa, na—na kutumia tu itikadi ndogondogo na mihemko na kadhalika, na kuiita hiyo Roho wa Mungu. Hiyo ndiyo sababu tumeaibika sana jinsi tulivyo siku hizi, mfumo mzima wa kanisa. Ni jambo baya sana. Na mbali na hayo yote, Yesu angali amesimama mlangoni, ametupwa nje.

¹⁷⁴ Lakini, hata hivyo, mlango mmoja zaidi ningetaka kufungua, mlango wa imani, kisha nitafunga. Kuna yapata dazani moja tu niliyoandika hapa, lakini nitairuka. Mlango wa imani.

¹⁷⁵ Mnasema, “Ungeweza kushuka uje kwenye Wafanyabiashara wa Full Gospel?”

“Ati nini?”

“Full Gospel.”

“Hiyo ni kinyume na imani yangu.”

¹⁷⁶ Kuna Imani moja tu. Hiyo ni kweli. “Imani moja, Bwana mmoja, ubatizo mmoja.” Hiyo ni kweli.

“Mbona, ni kinyume na imani yangu.”

¹⁷⁷ Labda humtaki Yesu kusimama katika mlango huo wa imani yako. Umejenga imani yako juu ya kanuni fulani ya imani ya kanisa fulani, dhehebu fulani. Na hapo ndipo imani yako imejifungia yenyewe, chumbani, wala usingeweza kumuruhusu Yesu kuja, ambaye ni Neno.

¹⁷⁸ “Hapo mwanzo alikuwako Neno,” ilisema Yohana Mtakatifu 1. “Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno akafanyika mwili akakaa miongoni mwetu.” Yeye ndiye Neno la Milele.

¹⁷⁹ Nawe, imani yako, ambayo—ambayo inasema, ya kwamba, “Siku za miujiza zimepita. Wala hakuna kitu kama kunena kwa lugha, na kutabiri. Na upuuzi huu ambao kanisa ama Wapentekoste hupiga makelele, siku hizi, hakuna kitu kama hicho.” Labda umeachilia kanuni fulani ya imani iufunge mlango wa imani yako.

¹⁸⁰ Laiti ungaliufungua mlango huo na kuliacha Neno la Mungu liingie, liwe Bwana wako, useme, “Sijali yale kanuni ya imani isemayo. Kama Biblia inasema hivyo, Wewe ni Bwana wangu.”

¹⁸¹ Huna budi kuzaliwa mara ya pili. Ndipo hapo unapozaliwa mara ya pili, basi huna budi kujazwa na Roho Mtakatifu. Haijalishi ni kanuni ipi ya imani, kile kilicho, hakuna kitu kuihusu.

¹⁸² Unasema, “Vema, ninaamini ya kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu.” Ibilisi anaamini jambo lile lile.

¹⁸³ Huna budi kuzaliwa mara ya pili. Kila mtu anaogopa huko Kuzaliwa upya. Loo, ninajua unajiita, kwamba una Kuzaliwa upya. Lakini nafikiri maisha yetu wakati mwingine hunena kwa sauti kubwa sana hata ushuhuda wetu hauwezi kusikika. Mnaona?

¹⁸⁴ Kuzaliwa ni mchafuko, sijali kuko wapi. Samahani tamshi hili, lakini kama kuzaliwa kumo katika kizizi cha nguruwe, ni mchafuko. Kama kuko katika banda la ng’ombe, ni mchafuko. Kama kuko katika chumba cha hospitalini, ni mchafuko. Na kama kuko madhabahuni, ni mchafuko. Kutakufanya uoze, katika mawazo yako mwenyewe. Kutakufanya utupilie mbali kila kitu ambacho... Vitu ambavyo wakati mmoja ulivipenda kwa moyo wako wote, utaviacha upate kuruhusu ule mbisho mdogo mtulivu. Sijali kama ni misheni huko pembeni.

¹⁸⁵ Sisi watu hapa nje tunaamini katika mambo makubwa. Sisi Wamarekani, tunataka kofia kubwa kubwa, na—na motokaa kubwa kubwa, na madhehebu makubwa, zaidi katika kanuni ya imani, na zaidi katika dhehebu. Yote tunayotaka ni mambo makubwa makubwa; naye Mungu anatafuta sauti ndogo, tulivu. Ghasia nyingi na makelele ndiyo tunayotaka.

¹⁸⁶ Mkulima alichukua mkokoteni wakati mmoja, akaenda shambani. Basi alipofanya hivyo, uligongagonga na kuchacharika na kufanya kelele nyingi sana. Uliporudi, ulipitia kwenye matuta yale wala hata haukutikisika. Ulikuwa umejaa vitu vizuri.

¹⁸⁷ Tunataka kanuni ya imani. “Dhehebu letu ndilo kubwa kuliko yote. Tuna *hili*. Utukufu kwa Mungu, tunalishinda kundi hili *hapa*. Tunalishinda kundi hili *hapa*, katika kulipa fedha, na kutoa nyota, na kila kitu kingine, kwamba ni nani atakayewaleta wengi zaidi kanisani.” Hakuna kitu dhidi ya hilo. Hilo ni sawa. Lakini, hili hapa ninalojaribu kusema, hilo Silo, bado. Hilo ni sawa, waleteni watu kanisani. Naam.

¹⁸⁸ Lakini Yesu alisema, “Wakati mtu alipotoka akaenda na kuongoa na kuleta mmoja,” kasema, “alifanyika nini? Maradufu mwana wa kuzimu kuliko alivyokuwa alipoanza.”

¹⁸⁹ Tunasikia, kwenye vipindi vya Billy Graham. Ambalo, sina la kusema dhidi ya mwinjilisti huyu mashuhuri. Bila shaka sina. Yeye ni mtu wa Mungu, naye Mungu anamtumia. Lakini yeye yuko wapi? Huko chini Sodoma. Mnakumbuka ule mfano? Kulikuwako na Malaika wawili walioshuka Sodoma, mfano

ambao Yesu alisema ingekuwa ni jambo lile lile katika Kuja Kwake.

¹⁹⁰ Lakini Mmoja alikaa pamoja na Ibrahimu, Kanisa teule, lililoitwa litoke. Angalieni kile Malaika wote wawili walichofanya, ndipo mmeepata Ujumbe.

¹⁹¹ Hivi si ni jambo la kigeni, kuwahusu wale wajumbe wawili? Jinsi hasa Mungu alivyosema, katika siku za mwisho, hapajakuwapo na mtu huko nje hudumani, katika siku zote za Moody, Sankey, Finney, Knox, Calvin, kotekote kuendelea chini, hapajakuwapo na mmoja ambaye jina lake liliishia kwa h-a-m, G-r-a-h-a-m, mpaka kwenye siku hii. Angalieni mjumbe kwa kanisa la kawaida, angalieni, “baba wa mataifa.”

¹⁹² Sasa, Kanisa la kiroho halikuwa kule, hapo mwanzo. Pentekoste, ikifananishwa, mwangalieni yule mjumbe akija kwa Kanisa *hilo*.

Yeye aliketi na kuzungumza na Ibrahimu. Akasema, “Yu wapi mkeo, Sara?” Naye akamwita “Ibrahimu.” Ambapo, jina lake lilikuwa ni Abram. Kasema, “Yu wapi mkeo, Sara?” Jina lake lilikuwa S-a-r-a-i, sasa ni S-a-r-a. Yeye aliita S-a-r-a.

Akasema, “Yuko hemani, nyuma Yako. Nyuma Yako.”

¹⁹³ Akasema, “Mimi,” kiwakilishi nafsi, “nitakutembelea, kulingana na majira ya uhai.” Naye Sara . . . Yeye alisema, “Kwa nini Sara akacheka niliposema hivyo?” Huyu hapo.

¹⁹⁴ Kwa nini iwe hivyo? Hatuna budi kuwa na roho kama huyo akizuru Kanisa, roho wa unabii, roho wa upambanuzi. Basi anapokuja, watu wanamkataa. Kwa nini? Ni Laodikia. Tumeshindiliwa sana kanuni za imani na kadhalika hata hatuwezi kumkubali. Hiyo ni kweli. Mnaona? “Nasimama mlangoni nabisha. Mtu yeyote akiisikia Sauti Yangu . . .”

¹⁹⁵ “Loo, imani yangu haiyakubali Mambo hayo.” Basi unayo imani mbaya.

¹⁹⁶ Imani, mnajua, Imani halisi ya kweli ya Mungu, itaitikia kila ahadi ya Mungu kwa “amina,” Roho Mtakatifu halisi. Kwa sababu gani? Roho Mtakatifu aliandika Biblia. Inasema hivyo. “Watu wa kale, wakiongozwa na Roho Mtakatifu, waliandika Biblia.” Mnaona? Basi Roho Mtakatifu angeweza kuwa ndani yako, kisha ulikane Hilo? Haiwezekani.

¹⁹⁷ “Mifano ya utauwa,” nabii alisema, “nao wangezikana nguvu zake,” kuwaweka huru wanaume na wanawake kutokana na dhambi na mambo ya ulimwengu. Mungu na aturehemu. Loo! Imani fulani ya kidini uliyo nayo, ambayo inakana Neno la Mungu, iondokee. Acha Neno la Mungu liwe kweli. Naam, bwana.

¹⁹⁸ Angalia. Yeye alisema, “Uwe-. . .hujui ya kwamba uko uchi, mnyonge, maskini, mwenye mashaka, na kipofu? Wala

hujui.” Hiyo hapo sehemu yenye mashaka. Sasa tutafunga. Ninawatakeni mlipate hili, “Wala hujui.”

¹⁹⁹ Sasa, kama ukimwona mtu akishuka hapa kwenye barabara kuu, Mtaa wa Stone, ama baadhi ya mitaa hii mikuu, naye mwanamume huyo alikuwa maskini sana hakuwa na nguo zozote, naye alikuwa mnyonge, mwenye mashaka, wala hana nguo, uchi; ama mwanamke, uchi wa mnyama, na kipofu; naye hakujua. Sasa, kama huyo mwanamke alijua, ama huyo mwanamume alijua, wangejaribu kutafuta mahali pa kuingia, wapate nguo. Lakini wakati hawajui hilo, halafu ujaribu kwenda kuwaambia, wanasema, “Shika lako.”

²⁰⁰ Sasa hivyo ndivyo hasa Yesu Kristo alivyosema kanisa la Kipentekoste lingekuwa katika siku za mwisho, “vuguvugu,” nalo lingekuwa “tajiri.” Sisi ni karibu tajiri kama lolote la hayo. Ilikuwa kwamba, wakati tulipokuwa huko chini kwenye misheni, tulikuwa na wokovu. Sasa tumejitokeza na nyadhifa kubwa kubwa namna hii, na washiriki wengi zaidi, na mambo makubwa mazuri mno, ndipo tuko wapi? Kama tu hao wengine. Naye Yesu alisema hivyo.

²⁰¹ Lakini katikati ya hayo yote, Yeye anaendelea kubisha. [Ndugu Branham anagongagonga mimbarani—Mh.] “Mtu yeyote (mtu binafsi) akiisikia Sauti Yangu, na kufungua mlango, nitaingia. Nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja na Mimi.”

²⁰² Hapo ndipo tunapofikia. “Uchi, vipofu.” Vipofu, kwa kweli vipofu, vipofu kiroho. Usingeweza kuwaambia chochote.

²⁰³ Mwajua, tulilelewa maskini hohehahe, huko chini Kentucky. Babu yangu alikuwa ni mwindaji, na mwi—mwindaji aliyejulikana sana. Naye alikuwa akiwinda mnyama aitwae kuuni. Sijui kama ninyi watu hapa nje... Hamna maji ya kutosha Arizona kuwa na kuuni, nadhani. Lakini wao—wao wanao, huko chini, walikuwa na kuuni. Waliwawinda kuuni.

²⁰⁴ Ni wangapi wanaojua mwinda kuuni ni nani? Vema, hebu waangalieni Wakentaki humu ndani. Jamani! Vema. Vema, ninajisikia kana kwamba ningetoa koti langu sasa na kuhubiri muda kidogo. Kwa namna fulani nilikuwa nimefungwa kidogo, bali najisikia vizuri sana sasa. Jamani!

²⁰⁵ Ni wangapi wanaojua godoro la nyasi kavu ni nini? Hum! Hum! Vema, Tony, asante. Nimerudi nyumbani, hatimaye. A-ha. A-ha. Naam. Hilo ni sawa. Jamani!

²⁰⁶ Ugali, uji wa shayiri, loo, jamani, njegere macho meusi, na mboga za tanipu! Mmepata kula zozote? Loo, jamani! Hilo ni, sasa, sisi tuko sawa sasa. Naam, bwana. Hilo ni zuri.

²⁰⁷ Basi babu alikuwa akiwashika kuuni, naye angewatoa mafuta. Na ninii... Walikuwa na kopo dogo. Tulikuwa tukiweka kopo hilo dogo la hamira.

208 Mama alikuwa na moja aliyokata biskuti nayo, ninii... kwa kopo la hamira. Naye angeoka hizo biskuti kubwa mno. Ungeshika upande wa juu, nao upande wa chini ungeanguka; na kutia molasi ya mtama mle ndani, na kipande kikubwa cha siagi ya kujitengenezea. Ilikuwa ni nzuri sana. Ingekuwa nzuri sasa hivi. Basi kidogo nilipungukiwa na sukari ya rojorojo asubuhi ya leo. Kwa hiyo, mwajua, na kitu kama hicho kingefaa kweli.

209 Basi mama alikuwa akiichukua shahamu hii ya kuuni, na hiyo—hiyo ilikuwa ni tiba kwa yote nyumbani kwetu, hiyo na dawa ya kuchua ya seng'enge. Naye... Tungepata jeraha, nao wangemimina hiyo dawa ya kuchua ya seng'enge ndani yetu, na terafini. Ndipo wakati tungepata kitu kibaya, tungekunywa shahamu ya kuuni.

210 Nasi tulikuwa na chumba kimoja kidogo, na kuna da—dari. Ilitubidi kupanda vi—vipandio, namna *hii*. Uzio wa ngazi ulikuwa umetengenezwa kwa miti michanga. Nasi watoto tungelala kule juu ya godoro la nyasi kavu. Na halafu juu ya godoro hilo la nyasi kavu kulikuwako na kitanda cha manyoya, godoro la manyoya. Halafu viezeko vya kabati viliwekwa penye nuru ya mwezi, na kwa hiyo ingefanya tundu. Basi—basi theluji ingepulizia ndani, kwa hiyo yeye angetufunika kwa kipande cha turubai, kuizuia theluji kuingia nyusoni mwetu wakati wa usiku, kundi hili dogo la Wabranham. Nasi tungekwa wawili miguuni, na wawili kichwani, na wawili katikati. Tulikuwa tu na kila namna ya njia za kulala, kugaagaa mle ndani kama nguruwe wadogo, na kupashana joto.

211 Mara moja moja, mmoja wetu angetoka chini ya turubai hiyo, wakati upepo baridi ulipokuwa ukivuma, nasi tungeshikwa na mafua, na tungeipata machoni mwetu. Na, mwajua, kitu hicho kinachonata kinaingia machoni mwako. Mama alikiita “matongotongo.” Kasema, “Mnashikwa na matongotongo machoni mwenu.”

212 Vema, ningeamka asubuhi. Naye mama angesema, “Billy, shuka uje. Ni wakati wa kwenda shuleni.”

Nami ningesema, “Mama, nina matongotongo machoni mwangu. Siwezi kuona.”

213 Naye, Humpy, kaka yangu, angeamka. Jina lake lilikuwa ni Edward, nasi tulimwita Humpy, kwa utani tu. Naye angesema, “Nina matongotongo machoni mwangu.”

214 Ningesikia maskini kopo la shahamu ya kuuni likigonga stovu. Yeye angeiyeyusha yote. Ndipo mama angepanda vipandio, naye angeyasugua na kuyachua macho hayo. Na, amini usiamini, matongotongo yangetoka. Shahamu ya kuuni ilikuwa ni tiba ya yote kwa macho yenye matongotongo.

215 Lakini, nawaambia, kumekuja kipindi cha baridi kote kanisani, na shahamu ya kuuni kamwe haitafaa kitu. Lakini Yesu alisema, “Nakushauri ununue Dawa ya macho,” Roho

Mtakatifu. Mnakuwa kipofu sana, kanisa linakuwa, mpaka ha—haliwezi kumwona Mungu. Linaona tu dhehebu lake. Linaona tu kile ambacho linaweza kuona mbele yetu. Kamwe haliangalii huko ng'ambo kwenye Kuja kwa Bwana hivi karibuni. Shahamu ya kuuni kamwe haitasaidia hilo hata kidogo.

²¹⁶ Lakini dawa ya macho ya Roho Mtakatifu itayafungua macho yenu, nanyi mnaweza kutambua ya kwamba, Uwepo wa Yesu Kristo. Na Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Yeye ni Mungu, naye anaweza kuyatia macho yenu dawa kwa Roho Wake Mtakatifu. Utasahau kama ulikuwa ni Mmethodisti, ama Mbaptisti, ama wa Umoja, ama wa Uwili, ama wa Utatu, ama Church of God, ama Mnazarayo, ama Mpilgrim Holiness. Utakuwa Mkristo, aliyezaliwa mara ya pili, kwa Ufalme wa Mungu.

²¹⁷ Ungekuwa ni kitu fulani. Haitakubidi kujaribu kusema, “Vema, sina budi kufanya *hivi*.” Kuna kitu ndani yako kinachokusukuma mbele kulifanya. Lile shurutisho moyoni mwako hukuingiza kwa maombi. Upendo wa Kiungu hububujika katika utu wako wa ndani kabisa, hata huwezi kutulia. Mikutano ya maombi hububujika tu kutoka kwako, kama maji yatokayo kwenye kisima cha chemchemi.

²¹⁸ Nilizoea kupita, wakati nilipokuwa bwana nyama kwa miaka kadhaa, ningepita karibu na chemchemi kubwa ya kale. Nayo ingekuwa ikibubujika namna *hiyo*. Ni—niliketi chini, kwenye chemchemi hiyo siku moja, nami nikasema, “Kwa nini una furaha namna hii?” Loo, hayo maji yalikuwa ni matamu. Nami ninge—ningekunywa maji. Nami nikasema, “Ni kwa nini una furaha sana? Hivi una furaha kwa sababu sungura hunywa kutoka kwako?”

Kama angaliweza kuzungumza, angesema, “La.”

“Kwa sababu paa hunywa kutoka kwako?”

“La.”

“Kwa sababu mimi hunywa kutoka kwako?”

“La.”

²¹⁹ “Kwa nini una furaha hivi? Ni kitu gani kinachokufanya ububujike namna *hiyo*?”

²²⁰ Kama angaliweza kunena, angalisema, “Si mimi ninayebubujika, Ndugu Branham. Ni kitu fulani nyuma yangu, kinachonisukuma, kikinifanya nibubujike siku zote.”

²²¹ Tunajisukuma kufanya mambo. Lakini Roho Mtakatifu anapokuwa mle ndani, kwa upendo wa Kiungu tunayafanya. “Kwangu mimi kuishi ni Kristo, na kufa ni faida,” kasema Paulo. Hakika. Sasa hebu Upako Wake wa dawa uje machoni mwenu.

²²² Katika kufunga, sikusudii kuwashikilia hapa mpaka nyote mmechoka sana. Ndio wakati wangu wa kwanza, ama wakati

wa pili, pamoja nanyi, samahani kama nimeenda muda mrefu kupita kiasi. Hebu nifunge, basi, nikisema hivi.

223 Huku chini Kusini, tulikuwa na maskini ndugu mweusi wa Kipentekoste huko chini, ambaye kweli alikuwa ni mtumishi halisi wa Kristo. Kulikuwako na dada fulani mkongwe wa Kinegro aliyekuja kanisani. Naye alijazwa na Roho Mtakatifu, naye alikuwa ni mtu mzuri sana. Naye alikuwa na mume; alikuwa ni jamaa mzuri mzee. Jina lake lilikuwa . . . Walimwita Gabriel. Nasi tulimwita tu Gabe, kifupi.

224 Na kwa hiyo tusingeweza kumfanya ajiweke sawa na kanisa. Ha—hakutaka kuja kanisani kamwe. Alisema hivyo. Loo, nao hao wavulana huko chini kwenye chumba cha biliadi ambako alitumia wakati wake, kasema, “Hilo lilikuwa ni kundi la watakatifu wanaojibingirisha, na hamna kitu kwao.” Na jambo pekee Gabe alilopaswa kufanya lilikuwa, Jumapili asubuhi, angechukua fimbo yake ya biliadi na kushuka kwenye chumba cha biliadi, ama kitu fulani, na kuzunguka na hao wavulana.

225 Lakini mke wake alikuwa ni mtakatifu aliyejitoa kweli. Basi mke angeenda kanisani, naye angeomba, na kumsihi mchungaji na wote wamwombe Gabe. Kwa sababu, kwa kweli, ndani ya moyo wake, alikuwa ni mtu mzuri. Naye alikuwa akiendesha biashara ndogo kule, ndogo pembeni, biashara ndogo ya kupiga viatu rangi. Angepiga viatu rangi, na kupata pesa za kutosha kucheza biliadi. Mbona, alienda na kucheza biliadi. Kwa hiyo hakutaka kabisa kujiweka sawa na Injili. Ndipo mchungaji . . .

226 Maskini Gabe alipenda kuwinda sana. Kwa hiyo, mchungaji alikuwa ni mwindaji, pia, kwa hiyo angemchukua Gabe na kuenda kuwinda. Kwa hiyo, siku moja, baada ya siku nzima ya kutembea kwa vishindo kote nyikani na vinamasi, walikuwa njiani wakienda nyumbani alasiri hiyo. Na—nao walikuwa na mawindo mengi sana ilikuwa ni vigumu kuyabeba. Walikuwa na sungura na ndege, mwilini mwote, wakitembea. Ndipo wakafika kwenye maskini njia waliyoiua wakati wakija. Wakafika juu ya kilima, kisha wakashuka kwenye mji mdogo pale. Ilikuwa ni Jumamosi, nalo jua lilikuwa linashuka.

227 Ndipo ikawa mchungaji aliangalia huku na huku. Hakuwa amemsikia maskini Gabe akisema chochote kwa muda mrefu. Naye akaangalia kote. Basi Gabe alikuwa akiangalia juu ya mabega yake, kuelekea ku—kutua kwa jua, wakati likivuka upeo wa macho wa magharibi. Ndipo mchungaji akaangalia nyuma. Akaona Gabe hakuwa akisema chochote, bali alikuwa akiangalia nyuma huku anatembea. Na kwa hiyo mchungaji akatembea kwa dakika chache.

228 Ndipo baada ya kitambo kidogo, mkono mkubwa mweusi ukawekwa begani mwake. Basi wakati alipogeuka, katika mshangao, maskini Gabe alikuwa akimwangalia usoni, huku machozi yakitiririka mashavuni mwake, yakidondoka namna

hii. Yeye anasema, “Mchungaji, asubuhi wewe unaenda kunikuta moja kwa moja kwenye lile benchi la mwombolezaji.” Kasema, “Ndipo mimi ninakuja moja kwa moja kutoka kule, na kuketi karibu na mke wangu mwaminifu. Ndipo mimi ninaenda kubaki katika kanisa hilo mpaka Mungu atakaponiita nyumbani.”

²²⁹ Naye mchungaji, bila shaka, akageuka kwa mshangao. Akasema, “Gabe, nilitaka, na nilingojea, na kutamani, na kuomba, kwa miaka, kwa ajili ya jambo hili.” Akasema, “Gabe, yote yamekwisha?”

²³⁰ Akasema, “Naam, mchungaji, yamekwisha. Lakini mimi namtaka huyo Roho Mtakatifu, pia. Na mimi ninakuja kwenye benchi la mwombolezaji asubuhi, na mimi ninaenda kumpata Yeye, la sivyo mimi naenda kufia papo hapo.”

²³¹ Kasema, “Gabe, na—nathamini hili.” Kasema, “Ila ninataka kukuuliza jambo fulani, Gabe. Ni mahubiri gani niliyohubiri, ambayo yalikuviua kufanya jambo hili? Ningetaka kujua ni mahubiri gani niliyohubiri, kile nilichohubiri. Ama, ni wimbo gani kwaya iliimba, ambao—ambao ulikuviua kufanya uamuzi huu mkuu, Gabe?”

²³² Ndipo maskini mzee huyo Mnegro akamwangalia mchungaji, naye akasema, “Mchungaji,” akasema, “Hakika ninathamini kila mahubiri uliyohubiri.” Akasema, “Na—nathamini kila kitu ambacho umesema, mchungaji.” Akasema, “Nami ninathamini kila wimbo mzuri kwaya iliimba. Lakini, kasema, “mchungaji, haukuwa huo.” Akasema, “Unajua, nilikuwa nikiangalia jua likitua huko ng’ambo. Hivi ulijua ya kwamba jua langu na lako, pia, linashuka, nuru ya mwili wetu inaondoka?” Na hiyo ni kweli.

²³³ Ni kweli hapa asubuhi ya leo, wanaume. Jua linatua, linatua katika maisha yako na yangu. Nalo linatua kwa wakati, katika ustaarabu. Umekwisha. Naye amesimama mlangoni, [Ndugu Branham anagongagonga mimbarani—Mh.] akibisha, akitamani, akingojea. Mbisho huo mdogo, kitu fulani ndani ya moyo wako kinachosema, “Ni Mimi. Fungua sasa.” Huyo ni Yeye. Gabe alikuwa amesikiliza hilo, ndipo akageuka.

²³⁴ Akasema jambo lingine, “Mchungaji,” akasema, “unajua mimi si mzuri wa shabaha.” Akasema, “Nisingeweza kupiga chochote risasi. Unajua nisingeweza. Basi hebu angalia tu hapa kwenye mawindo, ya kutosha kunilisha mimi na mke wangu juma lote lijalo.” Kisha kasema, “Unajua, siwezi kupiga risasi chochote, lakini,” kasema, “Yeye alinipa mimi.” Kasema, “Ilitokea tu nikawazia: Hapana shaka Yeye ananipenda, la sivyo asingekuwa mwema sana hivi kwangu.” Mliwahi kutambua hilo?

²³⁵ Huko India, leo hii, watoto wadogo, ninajua, wamelala mitaani, nayo maskini matumbo yao yamevimba, maskini fizi zao zimesinyaa *hivi*, wakifa kwa njaa. Maskini mama akisihi

huyu achukuliwe, na kuna maelfu zaidi. Ifikapo alasiri, wao huja na kuwaokota, katika machela na kadhalika, na kuwapeleka kwenye salamanda na kuwatupa mle. Hamna “Yohana 14.” Wanakula chochote, nyasi kutoka ardhini, ganda kutoka mtini, ama chochote wawezacho.

²³⁶ Sisi tunakusanya vya kutosha, katika mapipa yetu ya takataka, kuwalisha. Tumeketi hapa asubuhi ya leo, tukilipia kama dola moja na nusu kwa chakula kidogo hapa. Pia tuna nguo nzuri. Tunaendesha motokaa nzuri. Tunaishi katika nyumba nzuri. Ninyi wafanyabiashara hapa, biashara zenu zinastawi, kama ninavyosikia mkishuhudia. Mungu ni mwema kwenu. Hivi hamwezi kutambua hilo?

²³⁷ Mbona, Yeye anawapenda. Mnajua hilo? Na hiyo ndiyo sababu mbisho huo huja, “Nasimama mlangoni nabisha. [Ndugu Branham anagongagonga mimbara—Mh.] Na kama mtu yeyote atasikia Sauti Yangu, na kufungua mlango, nitaingia kwake, na kula pamoja naye, naye pamoja Nami.”

²³⁸ Sasa, ile Sauti ndogo, tulivu inayoubisha mlango wako wa moyo, huenda ikabisha mara nyingi sana hata huenda ikawa ni dhaifu sana sasa hivi. Lakini hebu tuwe tu waaminifu, tuwe tu waaminifu kwa Mungu na sisi wenyewe, kwa dakika moja tu. Huo mbisho mdogo, huko ndani kabisa, uliosema, “Afadhali nidhibiti njia zangu. Afadhali niwe tofauti. Afadhali nijirekebishe. Ninajua kuna mambo ndani yangu. Ninaangalia hapa, ninayachunguza maisha yangu na Neno hili, nami ninaona nimekosea katika mambo mengi.” Angalieni kote, angalieni alivyo mwema; ni wema Wake unaobisha mlangoni.

²³⁹ Haijalishi tumefanya nini, jinsi tumetenda dhambi, jinsi ambavyo tumelikataa, jinsi gani tulisema, “Baadaye tatalifanya,” Yeye angali, katikati ya yote hayo, anabisha. [Ndugu Branham aligongagonga mimbarani—Mh.] “Na kama mwanamume yeyote ama mwanamke utaufungua tu moyo wako, nitaingia na kula.”

²⁴⁰ Hebu tuone kile Yeye anachotaka asubuhi ya leo, sivyo, tunapoviinamisha vichwa vyetu? [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

²⁴¹ “Loo, Yesu wangu, nakupenda, nakupenda. Loo, nipe neema ya kukupenda zaidi, Bwana.”

²⁴² “Ni kitu gani hicho kidogo kinachoendelea kuniambia, moyoni mwangu, ya kwamba, ‘Sina budi kuja karibu zaidi na Yesu?’ Ni kitu gani hicho?” Unataka kukifungulia Hicho mlango, asubuhi ya leo?

²⁴³ Sasa, huku kila kichwa kimeinamishwa, na kila jicho limefumbwa, tafadhali. Chini katika moyo wako, kuwa mwaminifu kabisa, kwa dakika moja tu.

244 Una mbisho mdogo sana mlangoni pako. Ninaenda kuomba, kwa dakika moja tu. Na, kwa uaminifu, ungetaka kujua kitu hicho kidogo cha kisiri moyoni mwako ni nini, ambacho ungetaka ku—kukikaribisha. Hivi ungetaka Yeye aingie, asubuhi ya leo? Useme, “Ndugu Branham, omba ya kwamba nitakuwa na imani na neema ya kuufungua moyo wangu na kumwacha aingie. Ninataka kujua Hiki ni nini, kinachobisha mlangoni pangu. Ninajua kuna kitu kinachobisha mle. Labda ni kutembea karibu zaidi. Labda ni huduma tofauti. Labda ni kujisalimisha mwenyewe. Labda ni kumpokea Roho Mtakatifu.”

245 Naomba umwinulie Mungu mkono wako, useme, “Mimi hapa, Bwana.” Mungu awabariki. Jambo ndilo hilo. Loo, ni kila mahali. “Nina mbisho mdogo mlangoni mwa moyo wangu.” Nakisia, asilimia sitini ama sabini ya watu.

Huku vichwa vyetu vimeinaishwa.

246 Sasa, Baba yetu wa Mbinguni, “Kuna Chemchemi,” kama alivyosema mshairi, “iliyojaa Damu itokayo kwenye mishipa ya Imanueli, ambamo wenye dhambi wakitumbukizwa chini ya Mafuriko hayo hupoteza waa lao la hatia. Yule mwizi aliyekuwa akifa alifurahia kuiona Chemchemi hiyo katika siku yake, na hapo nijalie mimi, nijapo mwovu kama yeye, nioshe dhambi zangu zote.”

247 Sasa, Baba, tunashukuru kwa ajili ya watu hawa. Na baadhi yao huenda, hapana shaka, wamekiri Ukristo kwa muda mrefu, bali wana i—imani halisi ya kutosha kuinua mikono yao. Vipi, Bwana, kama hawakuwa hata na imani ya kutosha kuinua mikono yao? Basi wamepita ukombozi. Wazieni mahali hapo, ambapo nafsi iliyopotea ingeweza kutangatanga ikaingia gizani, na ni kipofu kabisa wala haijui. Nao wanausia mbisho wa Mungu, nao wanauhuzunisha mara nyingi sana hata hatimaye hautabisha tena. Nao wanaokota kanuni ya imani ama kitu fulani, na kuishi nayo siku zao zilizobakia, kujikuta wameudhika kwenye ile Siku ya Hukumu.

248 Ninashukuru, Bwana, kwa ajili ya watu hawa ambao wangeinua mikono yao na kusema, “Nirehemu, Bwana. Ingia moyoni mwangu, Bwana Yesu, na kujifunua Mwenyewe kwangu leo. Nami nitakupa maisha yangu. Mimi hapa. Kama kuna chochote ndani yangu ambacho si sahihi, Bwana... Nami ninayaangalia maisha yangu mwenyewe, nami naona ya kwamba kuna makosa mengi sana, basi niingize kwenye nyumba Yako kuu ya kufinyanga na—na unifinyange, na uniondolee yote yaliyo ya kilimwengu na yasiyo ya kitauwa. Nami ninakushukuru Wewe, Bwana, kwamba sijafikia mahali ambapo nimeuvuka huo mstari, ambao unaweza, ambapo unavuka wala kamwe huwezi kurudi tena; kumhuzunisha Roho wa Mungu kwa mara ya mwisho, na sasa hakuna njia kamwe, ya kurudi.” Kama vile Yuda Iskariote na hao wengine, alivyomwuzwa

Bwana wake kwa vipande thelathini vya fedha. Nasi tunafanya hivyo siku hizi, kwa ajili ya umaarufu, na mahangaiko ya ulimwenguni, na mashirika ya kidini na madhehebu, na kanuni za imani. Tunamwiza tu kwa ajili ya chochote.

²⁴⁹ Ee Bwana, irehemu mioyo miaminifu. Ninawaombea hao, Bwana. Loo, kwa yote yaliyo ndani yangu, ninaomba rehema ya Kiungu. Basi nisikie, Bwana, nisikie. Basi jalia shauku hii kuu, pamoja na imani, na kujua ya kwamba Mungu ndiye aliyenena na mioyo yao. Ni Mungu ndiye anayefanya mambo haya. Pia jalia mlango wa moyo ufunguke sasa hivi, naye Yesu aingie ndani na kuwa Bwana wa hali ya mambo, akiuondoa ulimwengu wote na kuwafanya viumbe vipya katika Kristo Yesu.

²⁵⁰ Waponye walio wagonjwa, Bwana. Tukiona kwamba kuna mateso mengi sana, ninawaombea, Baba, ili kwamba sasa yule Tabibu mkuu ataugusa utu wao wa kimwili, pia, na kuufanya makazi Yake, mahali Pake pa kuishi, ambako anaweza kuinyosha mikono Yake kwa wito tu. Huo wito mdogo, mwepesi wa moyo, na Tabibu mkuu yuko kazini. Tujalie, Bwana. Tusikie leo. Bariki wote waliopo. Katika Jina la Bwana Yesu Kristo, tunaomba. Amina.

²⁵¹ Sasa, huku vichwa vyetu vimeinamishwa, kwa unyenyekevu sana, kwa upole, hebu tuimbe maskini wimbo huu wa kanisa, "Nampenda, nampenda kwani alinipenda kwanza." Na muamini sasa ya kwamba yale mmeomba, ya kwamba huo mbisho mdogo mtulivu uliokuwa moyoni mwako, Yesu ataingia sasa. Kwa utulivu, tunapouimba.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

²⁵² Sasa, huku vichwa vyetu vimeinamishwa. Wewe unayetaka kumkubali kama Bwana moyoni mwako, "Bwana, ondoa kila kitu sasa. Na tangu wakati huu, ninajiweka wakfu Kwako juu ya meza hii, Bwana, kwamba nitakutana na Wewe tena kwenye kile Chakula cha jioni kikuu cha Arusi. Ninayaweka wakfu maisha yangu Kwako, asubuhi ya leo, kwa hiyo nisaidie, Bwana wangu. Iwapo sijampokea Roho Mtakatifu bado, nitamtafuta mpaka Roho Mtakatifu halisi aingie na kuyasafisha maisha yangu, kunifanya kiumbe kipya katika Kristo Yesu. Ninakuahidi Wewe leo hii, Bwana, ninapojiweka wakfu Kwako juu ya meza hii. Katika Jina la Kristo, ninaahidi kufanya hivyo, ninapoinua mikono yangu."

²⁵³ Sasa, inueni mikono yenu, na kuimba huku macho yenu yamefumbwa sasa.

Na...

Mtajiweka wakfu wenyewe sasa?

...mpenda

Kwani a...

²⁵⁴ Mungu, turehemu. Baba, iangalie mikono hii, na utujalie, katika Jina la Yesu.

Na kununua wokovu wangu

Mtini Kalvari.

²⁵⁵ Sasa nawatakeni mnyoshe mikono yenu mezani na kupeana mikono na mtu fulani. Useme, "Mungu akubariki, msafiri. Nina furaha kuwa hapa pamoja nawe, asubuhi ya leo." Hiyo ni kweli. Kila mtu jichanganyishe tu, Mmethodisti, Mbaptisti, Mkatoliki, Mpresbiteri. "Mungu awabariki. Mungu awabariki." Jumbe wakati mwingine zinakatakata na ni ngumu, na sisi—sisi tunataka ku—kujisikia vizuri juu Yake.

²⁵⁶ Sasa, Mungu akubariki, ndugu. Mungu akubariki. Mungu akubariki, dada. Mungu akubariki, ndugu yangu, Mungu awe pamoja nawe. Mungu akubariki. Sawa. Ubarikiwe, Ndugu Tony.

²⁵⁷ Sasa hebu na tusimame kwa dakika moja tu, pamoja na mikono yetu na mioyo yetu kwa Mungu, Baba yetu.

²⁵⁸ Kanuni zo—zote, zo—zote, sasa tukiamini. Sasa, mkiisha kuomba, kumbukeni, Yesu alisema, "Mwombapo, aminini ya kwamba mnapokea yale mwombayo, nanyi mtapewa." Mnaamini hilo? Semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] "Ninaamini ya kwamba ninapokea yale niliyoomba. Niliyaweka wakfu maisha yangu kwa Yesu Kristo. Na tangu leo hii, na kuendelea, kweli ninamaanisha hilo, Mungu. Nitatembea mbele Zako mpaka iwe uhalisi sana, mpaka nimefichwa kabisa katika Kristo Yesu."

²⁵⁹ Sasa, kiongozi wa nyimbo yupo hapa? Hebu tuanze wimbo huo wa kale wa neema, "Imani yangu inakutazama Wewe, Ewe Mwana-kondoo wa Kalvari, Mwokozi wa Kiungu." Sijui kama dada kwenye piano angeweza kutupa sauti hiyo. Ni wangapi wanaoujua huo wimbo? Inua... Sasa, hebu tuuimbe huo kwa sauti yetu yote, "Imani yangu inakutazama Wewe, Ewe Mwana-Kondoo wa Kalvari." Sote pamoja sasa.

Imani yangu inakutazama Wewe,

Ewe Mwana-kondoo wa Kalvari,

Ee Mwokozi wa Kiungu;

Nisikie sasa niombapo,

Ondoa dhambi zangu zote,

Loo nijalie tangu leo

Niwe Wako kabisa.

Hebu na tuinamishe vichwa vyetu sasa.

Wakati nikitembea kwenye mzingile wenye

giza la maisha,

Na huzuni zimenizunguka,

Kumbukeni, mnaenda kukabiliana na ulimwengu sasa.

Kuwa Kiongozi wangu; (Sikilizeni.)
Agiza giza libadilike liwe mchana,
Osha na kuondolea mbali woga wangu wote,
Wala usiniache kamwe nikachepuka
Kutoka Kwako.

²⁶⁰ Hebu tuuvumishe. [Ndugu Branham pamoja na kusanyiko wanaanza kuvumisha *Imani Yangu Inakutazama Wewe—Mh.*]



MLANGO KATIKA MLANGO SWA63-0223

(A Door In A Door)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumamosi asubuhi, tarehe 23 Februari, 1963, kwa ajili ya kiamshakinywa cha mkutano wa Kimataifa wa Wafanyabiashara wa Full Gospel katika Hoteli ya Ramada huko Tucson, Arizona, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2020 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org